

KUVAA SILAHA

ZOTE ZA MUNGU



Asante sana, Ndugu Ben. Asante sana.

Mnaweza kuketi, marafiki.

² Asante, Ndugu Vayle, hiyo ni . . . Sistahili u—utambulisho mdogo wa namna hiyo, bali hakika ninayathamini maneno hayo mazuri. Ingenibidi kuishi maisha makubwa ili kuishia huo.

³ Na kwa hiyo, nina furaha kuwa hapa, usiku wa leo, katika Pines Kusini, Carolina Kaskazini. Daima mimi huchanganyikiwa na hilo. Kama ni Carolina ya Kaskazini . . . [Ndugu mmoja anasema, “Kwa kweli huku ni Aberdeen, Ndugu Branham.”—Mh.] Wasemaje? [“Kwa kweli huku ni Aberdeen, hapa.”] Aberdeen, Aberdeen. Ninaposikia hiyo Pines Kusini inaonekana kwangu kana kwamba inapaswa kuwa Carolina Kusini, lakini ni Pines Kusini katika Carolina ya Kaskazini, ninachanganyikiwa kabisa.

⁴ Na, nina furaha tu kuwa hapa hata hivyo, na kuwa na wakati huu wa ushirika pamoja na marafiki zangu wa thamani, Ndugu Parker, Ndugu Lee Vayle, loo, hao wote, na wale wote wanaokaa hapa, wakingojea kuja kwa Bwana.

⁵ Na mimi—mimi kwa kweli sikumjua Ndugu Parker vizuri kama nilivyotaka, siku moja nilikuwa nikisoma makala katika gazeti, nami nikasema, “Thomas Parker, ninapaswa kujua jina hilo.” Ndipo kitambo kidogo tu, loo, ningesema siku moja au kitu kama hicho, Ndugu Lee Vayle akaingia, kasema, “Mbona, unajua huyo ni nani, huyo ni rafiki yetu kule juu.” Na kwa hiyo tukajaribu kumpata kwenye simu, nami nilitaka kumshukuru kwa maoni ambayo alikuwa ameyaandika gazetini. Na kwa hiyo basi, hivyo ndivyo tulivyopata kuunganishwa nipate kuwa hapa usiku wa leo kumsaidia katika mkutano huu mkubwa.

⁶ Nina furaha sana kuwa hapa, Ndugu Thomas, na kukutana na marafiki hawa wote wazuri, na kila mtu tena, na kuwa na wakati wa ushirika. Lakini mnaweza kuwazia jinsi ninavyojisikia kusimama hapa usiku wa leo, kuhubiri Ujumbe wa Biblia, huku watu kama hao wameketi nyuma yangu.

⁷ Kwa kweli, ninahisi kitu fulani . . . Labda afadhali nifanye kama Dwight Moody, walisema alifanya hivyo alipokuwa Uingereza, alikuwa akizungumza usiku mmoja mbele ya Wakukni, ambao kweli hutamka maneno yao vizuri sana, naye Bw. Moody hakuwa na elimu, kwa hiyo alijaribu kusoma Andiko, naye akatamka vibaya maneno matatu ama manne,

ndipo akarudi na kulijaribu tena naye akalitamka vibaya kuliko hapo awali, kwa hiyo akaifunga tu Biblia, na kuangalia juu Mbinguni, na kusema, “Mungu, nisaidie,” ndipo akaitikisa hiyo nchi. Kwa hiyo hivyo—hivyo ndivyo ilivyo. Mtazame tu Yeye, na hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya.

⁸ Nao huu mkutano mkubwa, nadhani wote umetangazwa, unaendelea hapa juu maskanini, Maskani ya Biblia, ninaamini ndivyo inavyoitwa. Nami nina hakika kama mtapanda kwenda kule, enyi marafiki, bila shaka mtasikia jambo fulani. Nimesoma makala mengi, lakini Ndugu Thomas anatokea kuwa miongoni mwa waandishi mashuhuri, nafikiri, wa siku hizi, mshiko wake wa Neno la Mungu. Halafu basi, nina hakika mtanufaika kwenda huko.

⁹ Huenda kidogo nikaonekana nimejeruhiwa, usiku wa leo, usoni mwangu, na machoni mwangu. Nadhani tayari mmesikia kwamba nilikuwa nikipiga risasi yapata majuma manne yaliyopita, na . . . Burudani yangu sikuzote ilikuwa ni kuvua samaki, kuwinda, ama—ama chochote kile, na, namna hiyo, porini, kamwe sijawahi kucheza gofu, wala mpira, wala mbio za farasi, na chochote kile, ninapenda tu mambo ya porini, nami ninapenda sana.

¹⁰ Nilipokuwa Afrika kwa namna fulani nilizipenda bunduki za Roy Weatherby, lakini kamwe nisingeweza kuwazia ningeweza kumudu moja ya hizo. Na kwa hiyo walikuwa . . . Baadhi ya marafiki zangu labda wangeninunulia moja kama ningewaruhusu, lakini nisingewaruhusu, kama nilivyomwambia Ndugu Thomas alasiri ya leo, nisingeweza kuwazia kuwaruhusu baadhi ya marafiki zangu kuninunulia moja ya hizo bunduki za bei ghali, wakati ninajua wamishenari wasio na viatu miguuni mwao, nisingeweza kujisikia vizuri na hiyo bunduki.

¹¹ Kwa hiyo rafiki yangu akaja, nami nilikuwa na bunduki nyingine pale ambayo mtu fulani alimpa Billy Paul, naye aliendesha Kampuni ya Weatherby huko Indiana, naye akasema, “Hebu niipeleke ikatobolewe kwa ajili yako, na kuifanya bunduki ya Weatherby.”

¹² Vema, ilitokea kwamba, hawakuitoboa vizuri, nikatia risasi niifyatue, yapata tani sita za mlipuko papo hapo usoni mwangu, na urefu wa kama mapazia yale, moto mwekundu tu, nao mtutu ukafikia kwenye mstari wa yadi hamsini, tako likaenda *hivi*, nayo bunduki ikayeyukia mikononi mwangu.

¹³ Nami nisingeweza kuona wala kusikia chochote kwa dakika chache. Basi wakati nilipoweza, kuifungua mikono yangu namna *hii*, kuyafungua macho yangu, jicho *hili* upande *huu*, ningeweza kuona damu ikitiririka namna *hiyo*. Nami nikainua mkono wangu juu *hivi*, nalo jino *hili* likang’olewa *hapa* ambapo kile kipande cha marisau kiliingilia, kikatoboa duara kubwa usoni mwangu, ndipo vipande kumi na vitano vikafanya nusu mwezi

papa hapa chini ya jicho langu na vikaenda mpaka nyuma ya mboni ya jicho, lakini kamwe hayakugusa sehemu ya kuonea.

¹⁴ Na kwa hiyo wakati daktari aliponichunguza, waliponipeleka kule, alisema, “Jambo pekee nijualo, Bwana mwema hapana shaka alikuwa ameketi pale pamoja na mtumishi Wake la sivyo hata usingekuwa na kichwa wala mabega, kwa mlipuko huo wote.”

¹⁵ Kwa hivyo hizi zote ni siku nzuri na wakati mzuri kwangu. Ni—nina furaha kuwa hapa. Ninii tu... Kwa hiyo ninajisikia kwa hilo, ya kwamba Bwana hakuwa amemaliza nami bado. Na labda ananitaka nijaribu kuwatetea watu Wake zaidi kidogo na kujaribu kusaidia. Nami nipo hapa kufanya yote niweza ya kuwarahisishia maisha kidogo, na kujaribu kuwasaidia vizuri nijuavyo. Kwa hiyo mtaniombea, nina hakika.

¹⁶ Na... [Ndugu Vayle anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Naam. Naam, bwana. Naam, bwana.) Ndugu Vayle alikuwa tu akiniambia ya kwamba kipaza sauti hapa, ndicho pekee... kina maikrofoni ndogo tu. Mnaweza kusikia huko nyuma vizuri? Mnaweza kusikia. Hilo ni zuri.

¹⁷ Kwa hiyo sikupoteza kuona kwangu, wala kusikia kwangu. Bado nina kipenga cha kujificha hapa mahali fulani. Nalo jicho hili la kulia lina uastigimati ndani yake, nadhani hivyo ndivyo unavyolitamka, lina wasiwasi, linatetemeka. Lakini litapata nafuu, litakuwa sawa tu, kwa hiyo kila kitu kitakuwa sawa na kizuri. Nami najua ilikuwa ni kwa kusudi fulani. Tunajua ya kwamba Bwana wetu daima ni wa kweli, wakati aliposema angefanya kila kitu kitende kazi hivyo. Kwa hiyo ninamtumainia tu Yeye kuwa hivyo.

¹⁸ Yeye ameniambia mambo mengi, na kunijalia kukwepa matatizo mengi, lakini mwajua, hawezi kuniruhusu kuyakwepa yote. Hatuna budi, sisi wahudumu hatuna budi kuteseka vile vile kama ninyi watu huko. Bwana wakati mwingine hunena na kutujulisha jinsi ya kuepukana na matatizo, na kufanya mambo, lakini kumbukeni, tunaingia moja kwa moja kwenye sehemu hizo pia, ambako inatubidi kuteseka pamoja na hao wengine. Na kwa kweli ni vigumu zaidi kwetu kuliko ilivyo kwenu, inaonekana kana kwamba Yeye anashikilia kwa muda mrefu kwa ajili yetu, mwajua, hajibu wakati wote. Kwa hiyo lakini tunashukuru kwamba Yeye daima huja akipanda wimbi, na kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya hilo.

¹⁹ Kila mtu anajisikia vizuri? Jamani, jamani, huo unasikika kama ni mkutano mkubwa kweli, yaani, na, kila mtu yuko sawa. Ombeni sasa, na usiku wa leo, nilitoa muktadha mdogo hapa kutoka kwenye kile kinachoweza kuitwa somo ninalotaka kusoma. Nami nina Maandiko na muhtasari kidogo ulioandikwa hapa, ambao ningetaka kufanya darasa dogo la shule ya Jumapili kutoka kwake, kitu kama hicho.

²⁰ Halafu ningetaka tu kuuliza . . . Bila shaka, kwa kawaida mwanzoni, hakuna wengi sana hapa, labda ningeweza, kukiweko na watu wagonjwa wa kuombewa, ningeweza kufanyiza mstari wa maombi na kushika kila mmoja wao katika usiku mmoja. Kwa hiyo labda nitaanza, kuuliza usiku wa leo, na kuona ni wangapi waliokuwa hapa wapate kuombewa, na kwa namna fulani mmekuja mkutanoni, mnataka maombi kwa ajili ya miili yenu iliyo migonjwa na mnetaka tuwaombee. Waweza tu kuinua mkono wako, useme, “Nimekuja kwa kusudi hilo”? Vema, hilo ni zuri sana, hilo ni sawa, angalieni hilo usiku wa kwanza. Kwa kawaida watu kwa namna fulani hungojea mpaka mwisho, ndipo kidogo ni vigumu.

²¹ Ni vema sana kuwaona hapa mkimwamini Mungu, kwamba mnaamini ya kwamba Mungu atajibu, Atajibu, Yeye hashindwi, kamwe hatashindwa. “Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humponya nayo yote.” Kwa hiyo maadamu tu tunapata ukombozi, ndilo jambo kuu. Nasi tunaingia mitegoni wakati mwingine, kama vile Paulo na hao wengine ambao wametutangulia, wale watakatifu wakuu na wateule wa Mungu, na sisi ni . . . tunajua hatuwezi kuomba tuyakwepe matatizo, lakini daima kuna kitu fulani nyuma yake kwamba Mungu huyafanya yatende kazi vizuri kwa ajili yetu sote.

²² Ninaamini dakika chache zilizopita, sijakosea, ninamwona rafiki yangu mwema, Ndugu Sullivan, anayeketi hapa chini pia, wote, kutoka huko chini Kentucky. Nina furaha kukuona, Ndugu Sullivan. Na, Ndugu Iverson, Florida. Loo, kila mahali! Na ni wangapi walio hapa kutoka nje ya mji? Hebu tuone mikono yenu, kutoka kwenye hii. . . Vema, tuseme, kuna mtu yeyote hapa kutoka mjini? Hebu tuone mikono yenu, kutoka mjini, kutoka karibu na mji? Loo, mnajua nini! Yapata watu kumi na wawili, kumi na watano, ninaoawaona. Huo ni u—uwakilishi mzuri kutoka nje ya mji, Ndugu. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo mikusanyiko mikubwa inavyovutia kwa kawaida.

Vema, mke wangu alizoea kuniambia wimbo mdogo:

Watatoka Mashariki na Magharibi,
Watakuja kutoka nchi za mbali,
Kula pamoja na Mfalme wetu,
Kula kama mgeni Wake;
Jinsi hawa wasafiri walivyobarikiwa!
Wakiutazama uso Wake uliotukuka
Unaowaka kwa upendo wa Kiungu;
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Kama vito katika taji Yake kuangaza.

Mnaujua huo wimbo?

Yesu yuaja upesi,
Majaribu yetu yataisha basi.

Loo, vipi kama Bwana wetu angekuja wakati huu

Kwa ajili ya wale walio huru na dhambi?

Basi ingekuletea furaha,

Au huzuni au kukata tamaa kabisa?

Bwana wetu ajapo katika utukufu,

Tutamlaki juu hewani.

²³ Hilo ndilo kusudi letu la kuwa hapa. Sasa, mimi si mwimbaji, marafiki, ni—nisingeweza kuimba. Mimi... Mnajua, sikuzote nimetaka kuimba, Ndugu. Kwa hiyo nitawaambieni nyote, wakati mwingine mnaweza kunisikia nikiimba wakati ninapoweza kuimba: Mtakapofika Mbinguni, na yote yamekwisha, nanyi mko katika majumba yenu makuu (Sikuzote nimependa misitu sana na kadhalika, labda nina kibanda kidogo huko chini pembeni mwa nchi ya Utukufu mahali fulani.), ukitoka nje ukumbizoni mwa jumba lako kubwa asubuhi moja, ama baraza, usikilize, huko chini kabisa mwituni usikie sauti ikija, ikiimba “Ni neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu.” Useme, “Ndugu Branham alifaulu.”

²⁴ Endapo, wakati Yeye anaweza kumchukua mnyonge kama mimi na kuniokoa, mbona, basi kuna tumaini kwa ajili yetu sote. Nawe utaona, useme tu, “Ndugu Branham alifaulu, maana huyo hapo, angali anaimba *Neema ya Ajabu*.” Sikuzote nilitaka kuuimba huo, ninaweza tu kuuvumisha moyoni mwangu, bali natumaini siku moja kweli ninaweza kuuimba.

²⁵ Hebu tufungue Waefeso mlango wa 6. Na hapa umekaribia wakati wa kutoka, nasi ndio tu tunaanza. Waefeso mlango wa 6, tunaanza na kifungu cha 10 na kusoma sehemu ya Neno:

Hatimaye, ndugu zangu, mzidi kuwa hodari katika Bwana, na katika uweza wa nguvu zake.

Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.

Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa... giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.

Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana... ninii... siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.

Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na mna... dirii ya haki kifuari;

Na kufunguwa miguu utayari tupatao kwa injili ya amani;

Na zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima... mishale yenye moto ya yule mwovu.

Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, . . . upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu:

Kwa sala zote na maombi . . . mkisali kila wakati kwa maombi katika . . . Roho, . . . mkikeshwa huko kwa uvumilivu wote na kudumu katika kuwaombea . . . watakatifu wote;

²⁶ Ningetaka kuchukua somo kutoka kwenye hilo, *Kuvaa Silaha Zote Za Mungu*. Nami nilikuwa nikiwazia muda mfupi uliopita ya kwamba hili huenda likafaa kwa namna fulani kuliingilia kidogo kwa ajili ya ujumbe kwa ajili ya kesho asubuhi, na kwa ajili ya siku zifuatazo hapa mkutanoni, kwa sababu kwa kawaida ni kwenye mkutano ambapo watu hawa mashuhuri, walioitwa kwa ajili ya mafundisho haya, kwa kawaida huwapelekea watu Ne—Neno.

²⁷ Na kwa hiyo, Paulo hapa anazungumza juu ya mavazi ya askari, akienda vitani, askari akivaa silaha, akijiandaa kwa ajili ya vi—vita. Na kwa namna fulani napenda jinsi anavyoiweka, maandalizi.

²⁸ Mnajua, ninaamini ilikuwa ni Lincoln aliyesema wakati mmoja, “Wakati wa amani, jiandaeni kwa vita.” Ama, huenda haikuwa ni yeye, lakini inaonekana hivyo, inaonekana kwangu, hasa, ndiye aliyetoa msemo huo. “Wakati wa amani, jiandaeni kwa vita.” Na hilo lingekuwa ni jambo zuri kwetu kuwazia. Wakati ambapo kila kitu kinaendelea vizuri, afadhali uwe tayari, kwa maana Shetani hataiacha iendeleo vizuri kwa muda mrefu sana.

²⁹ Uko mkutanoni sasa, na kila kitu kitatiririka vizuri, lakini utaondoka hapa katika siku chache, nawe utakutana na adui. Huenda . . . huenda hata asingoje mpaka uwe tayari kuondoka, a—anaweza kushambulia wakati wowote, kwa hiyo ye—yeye ni mwovu na katili, yeye huendeleza tu lolote awezalo, lolote awezalo kusema ama kufanya, hulifanya sasa hivi, yeye . . . Kwa hiyo ni bora zaidi kuvaa silaha wakati wote.

³⁰ Huenda ukakutana naye huko nje mtaani, huenda ukakutana naye katika ninii yako . . . kwenye gari, ni vigumu kusema mahali utakapokutana naye, ama atakutana nawe moja kwa moja hapo kitini, nami papa hapa mimbarani, mahali popote. Yeye ni—yeye ni mwovu tu, wala hajali, kwa hiyo tunataka kuwa tayari kwa ajili yake.

³¹ Naye mwalimu huyu mashuhuri, Mtakatifu Paulo, alikuwa akilifundisha Kanisa jinsi ya kuvaa silaha, naye alikuwa akililinganisha na askari anayejitayarisha kwa ajili ya vita vikuu vilivyo mbele.

³² Sasa, tunaona karibu, katika mataifa, kuna mara nyingi ambapo mataifa, haidhuru kama wao ni marafiki ama si marafiki, kila taifa lina wapelelezi wake. Sasa, tuna wapelelezi wetu kote ulimwenguni, na kila taifa ulimwenguni lina

wapelelezi wao hapa, kama wao ni wa kirafiki ama si wa kirafiki; kwa namna fulani wanashuku kidogo, mwajua.

³³ Sasa, Uingereza ni moja ya mataifa wenzetu, lakini hata hivyo tuna wapelelezi huko Uingereza, Uingereza ina wapelelezi hapa. Tunao kila mahali. Hata hivyo... Kwa hiyo wanafanya mizunguko yao, nao ni marafiki, watu wazuri, kwa kweli hakuna kitu ungaliweza kusema dhidi yao, bali wako tu macho, wakiangalia, wakiona kinachoendelea, na kutazamia silaha mpya ambayo itatengenezwa.

³⁴ Nao watapenya moja kwa moja waone jinsi hiyo silaha ilivyo, kisha wataipeleka kwa nchi yao wenyewe, na—nao watajitayarisha kurudisha shambulizi. Kama tungetumia silaha hii, mbona, wangeweza *kutushambulia tena* nayo, ama kama tungetumia silaha zao, ama watumie silaha zao juu yetu, wapelelezi wetu. Nasi tutatengeneza silaha fulani za kushambulia silaha wanayopanga kutumia, ama siri fulani, majasusi, ama jambo fulani la siri tunalopanga kufanya.

³⁵ Nao watajitayarisha, kwa sababu wana wapelelezi hapa kwa kusudi hilo, kupeleleza na kuona yale tufanyayo, tuna wapelelezi kule, wanaopeleleza, wakiona yale wafanyayo. Inaonekana kana kwamba kwa kweli hatuwezi kuaminiana. Ninii tu, inaonekana tu kana kwamba kuna kitu fulani ndani ya wanadamu kinafikia *umbali huu*, huo ndio umbali tu kinachoweza kwenda.

³⁶ Nina furaha kuna Kitu tunachoweza kukiamini kabisa, sivyo? Kitu ambacho ni, haitubidi kushangaa, kuwazia, kujua tu ya kwamba tungeweza tu kupumzika kama watoto wadogo. Nafikiri hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa, hasa sana Wakristo. Tunapaswa kuwa kama...

³⁷ Hapo mwanzo unaona, mwanadamu anajaribu kupata mahali hapo, kwa sababu wakati alipoumbwa kwa mfanano wa Mungu kwa mara ya kwanza, haikumbidi kujitegemea, basi Mungu akamhudumia. Lakini kwa kuwa amekuwa m—mgeni, ama m—mzururaji, basi hana budi kujitegemea, naye anashuku kila kitu. Yeye ni ninii tu, kunradhi kwa tamshi hili, kwa namna fulani yeye ni mzuka, kila kitu kinaonekana kidogo kina tahadhari, ameondoka, hataki kukingojea.

³⁸ Sasa, mataifa hufanya mambo haya, wanapeleleza. Nao daima... Sababu ya kulazimika kufanya hivi, ni kwamba silaha zao za kale walizokuwa wakitumia hupitwa na wakati. Sasa, tungefanya nini na uta na mshale ambao walitumia wakati mmoja? Ama tungefanyaje na silaha za kale walizotumia katika Vita vya Kwanza vya Dunia? Bunduki ya kale ya Krag-Jørgensen? Ama tungefanya nini na Springfield? Hizo zimebadilishwa, vita vya mwisho na Garandi, vita hivi vyenye kombora la atomiki ndani yake. Mnaona, ni... zinapitwa na wakati.

³⁹ Ile ndege ya kale tuliyozea, Air Knocker, iliyotokea katika Vita vya Kwanza vya Dunia, mbona, walitumia ndege yenye injini tatu ama nne katika vita hivi vya mwisho. Na sasa, ni takataka tu, haifai kitu, imepitwa na wakati. Watumie mamilioni ya dola kuzitengeneza, halafu—halafu wazitupe kwenye chungu kikubwa cha kufinyanga, kuzifinyanga tena, kwa sababu kwamba adui, na wapelelezi wetu wanaoripoti, wameleta habari kwamba wana ndege kubwa zaidi. Sasa, tunasafiri kwa jeti.

⁴⁰ Sasa, wamefikia ambapo wanaweza kuilenga kwa nyota, wavute wenzu mmoja, na ulimwengu mzima ugeuke uwe wingu la mavumbi, kwa hiyo mwisho wa jambo hili umekaribia sana. Wala hakuna kitu wanachojua cha kufanya sasa. Silaha zote za kale zimebadilishwa zikawa mabaki.

⁴¹ Nilikuwa nikiwazia, lile gari-moshi la kale lililoendeshwa kwa makaa lililokuwa likichukua . . . lilipitia Jeffersonville pale karibu na depo, nayo yangekuwa na misururu mikubwa ya—ya bunduki, na kuzipeleka huko Fort Knox ambako zilikuwa zimetengenezewa, na vifaru. Lile garimoshi la kale ambalo . . . hakuna hata moja ya hayo kwenye reli tena, yote yamekwisha, nayo yamewekwa humu kama kumbukumbu. Waliyatumia katika vita hivi vya mwisho, lakini sasa ni ya dizeli. Katika siku chache tu yatakuwa ni ya kuendeshwa na atomiki. Kwa hiyo hayo yote tu, inawabidi kuyatupa kwenye takataka na kuanza tena.

⁴² Nanyi mnajua katika vita hivi kati ya mataifa, kuna vita vikuu vinavyoendelea zaidi ya hivyo, na hivyo ni vita kati ya Mungu na Shetani, vita vikuu. Na hivyo vilikuwa ndivyo vita vya kwanza, na vingali vimepamba moto. Lakini, loo, nina furaha sana hivi karibuni vitakwisha, na yote yatakwisha.

⁴³ Shetani ana mawakala wake kila mahali, wakiangalia, wakiwapeleleza watu wa Mungu, matendo ya Mungu. Ninii yake . . . Adui ameketi kila mahali, akiangalia, aone kile anachoweza kufanya. Naye Mungu ametoa wengine pia, kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo.

⁴⁴ Na kila taifa huandaa jeshi lake kwa vifaa bora sana vya kisasa zaidi liwezalo kupata. Hiyo ndiyo sababu mitambo yetu ya kale inapitwa na wakati, ni kwa sababu tunaona, kama vile Ujerumani kwenye rada, na—na vitu mbalimbali tunavyoviona kutoka kwa mataifa mengine, na kitu ambacho tunajibunia wenyewe.

⁴⁵ Sasa, wana mtu anayezungukazunguka angani. Wote wanapayuka—payuka kuhusu hilo mwajua, “Tuna mtu angani.” Mbona, hilo si kitu, sisi Wakristo tumekuwa na mmoja angani kwa miaka elfu mbili, mwajua. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Wanapiga makelele juu ya hilo, hilo si jambo jipya, hilo ni la kale

kwetu, tulijua hilo wakati wote. Kwa hiyo, mnaona? Mnaona, hivyo ndivyo tu tulivyo mbele sana, kamwe hawatambui.

⁴⁶ Naam, kujenga barabara kubwa mno na vitu vikuu namna hiyo na kujaribu kuifanya dunia kuwa mahali bora zaidi na kadhalika, hawatambui ya kwamba walio wapole watairithi, kwa hiyo haya basi. Kwa hiyo ninii tu—ninii tu... Mnaona, Mungu ameyawazia yote kwetu. Hilo ni, jambo pekee linalotupasa kufanya, ni kumshikilia tu na kuendelea tu mbele moja kwa moja. Mnaona? Hiyo ni, kuamini kabisa, hivyo tu ndivyo alivyotuomba tufanye, atatuvusha moja kwa moja.

⁴⁷ Kwa hiyo tunaona ya kwamba hawa mawakala wa siri wa adui wanaketi huku. Kila taifa sasa, litawapa watu wake vifaa vya kisasa kabisa, vya kisasa kabisa, nao wanasoma, na wanafanya kila kitu, wanajaribu kukabiliana na silaha ya hao jamaa wengine, na kupata si—silaha ya kisasa zaidi, kidogo, kitu fulani chenye nguvu zaidi kidogo. Kutoka kwa uta na mshale hadi gobori, na kutoka kwa gobori hadi bunduki ya kisasa, na kutoka hiyo hadi ya atomiki, wanaendelea tu kujenga, inawafanya kuwa na shughuli nyingi wakati wote, na ni shughuli ya taifa. Kama wanataka kuishi, wanataka kuwapa askari wao vifaa bora zaidi vilivyopo.

⁴⁸ Vema, Mungu, mnajua Yeye hana kikomo, mnaona, haimbidi kuwazia jambo lolote bora zaidi, alipata tu kilicho bora zaidi mwanzoni, kwa hiyo huwezi kuliboresha, hakuna kitu kinachoweza kufanywa juu yake. Yeye hutupa tu yaliyo bora zaidi, hilo ni Neno Lake. Amina. Hiyo ni kweli. Hilo ni Neno Lake, lililo bora zaidi linaloweza kutolewa.

⁴⁹ Mungu huwapa watu Wake kilicho bora zaidi, na hicho ndicho alichowachagulia watoto Wake, kilicho bora sana, sana. Nina furaha sana kwa jambo hilo. Ninamwona Mungu, Baba yetu, na Ufalme ambao sisi ni wajumbe wake.

⁵⁰ Yeye hana kikomo. Sasa, mataifa haya yanaendelea kujenga, na kusoma, na kufanya kazi, na kuendelea katika sayansi, na kila kitu namna hiyo, lakini, mnaona, Mungu, kwa kuwa hana kikomo, kwa hiyo Yeye anajua mwisho tangu mwanzo, na kabla halijatukia Yeye anajua jinsi gani, lini, na mahali gani. Kwa hiyo tunaweza kuwa na hakika ya kwamba maadamu tu tuko ndani Yake kila kitu kinaendelea vizuri kabisa. Hakuna haja ya kuogopa chochote, hakuna kitu kinachoweza kutusumbua. Kwa hiyo tunapumzika tu kwa amani kama watoto wadogo, wala hakuna kitu kinachoweza kutudhuru.

⁵¹ Kwa hiyo Mungu asiye na kikomo, mnaona, hiyo ndiyo sababu ninaamini Neno Lake, sivyo? Ni kwa sababu Neno hilo ni Yeye, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno, alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Sasa, kwa hiyo basi, Mungu alijua ya kwamba Mwenyewe asingeweza kushindwa

kwa sababu alikuwa juu ya Shetani, kwa hiyo Yeye alijitoa tu Mwenyewe, mnaona, Neno Lake, kwa hiyo huko ndiko kushindwa.

⁵² Sasa, Mungu hawezi kufanya uamuzi leo, na kesho arudi na kufanya uamuzi bora zaidi, mnaona, kwa sababu uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu, kamwe haimbidi kuubadilisha. Kwa hiyo basi tunaweza kutulia juu ya lolote Mungu asemalo, hiyo ndiyo sababu ninaamini Biblia ni Neno la Mungu.

⁵³ Sasa, sababu ya mimi kuamini jambo hilo, kwamba Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa Kigezo fulani. Na kama ni kwa kanisa, ni lipi? Mnaona, kuna mamia yao, na makanisa mbalimbali na madhehebu, vema. Lakini huwezi... Mlutheri asema, "*Tunayo*."

Naye Mbaptisti anasema, "La, *tunayo*."

Naye Mpresbiteri anasema, "*Tunayo*."

Naye Mpentekoste anasema, "La, *ndio huu*."

⁵⁴ Mnazarayo anasema, "La, *ndio huu*." Ungechanganyikiwa, lakini unaona, *Huo* ni Neno. Ni—ninaliamini tu, Neno. Mnaona? Lichukue tu jinsi lilivyoandikwa, liamini, wala si la kufasiriwa apendavyo mtu, linasema, limeandikwa tu mle.

⁵⁵ Ndipo basi kama hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa Kigezo fulani, mbona, *Hili*, Yeye amelilinda, kwa hiyo liko tu jinsi linavyopaswa kuwa. Kwa hiyo ninaliamini tu namna hiyo. Lisome tu, useme, "Naam, Bwana."

Nami ninaamini tunapomwamini Mungu, kila wakati Mungu anaposema jambo lolote, tunaliitikia kwa "Amina." Hiyo ni kweli, lolote alilosema Mungu.

Alisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, na hata milele."

Sasa, mtu fulani angesema, "Vema, kwa njia fulani."

Uh-uh! "Amina."

Kama Yeye alisema, "Tubuni mkabatizwe mkampokee Roho Mtakatifu."

"Amina." Mnaona?

Yeye alisema, "Mwenye haki ataishi kwa imani."

"Amina."

Naye akasema, "Nitakuja tena."

⁵⁶ "Amina." Na lolote asemalo, Roho Mtakatifu ndani yetu huliitikia tu kwa "Amina." Mnaona? Kisha angalia jambo linalofuata. Unaona? Sasa, ni...hilo ni zuri sana kwamba tunaweza kuwa na imani kama hiyo.

⁵⁷ Sasa, sababu ya mimi kujua ni sahihi ni kwa sababu Mungu alisema, katika Kitabu cha Ufunuo, "Mtu yeyote atakayeondoa sehemu moja kutoka katika Kitabu hiki, ama kuongeza sehemu

moja Kwake!” Loo, jamani, Hilo halina budi kuwa ndilo atakalouhukumu ulimwengu kwalo basi.

⁵⁸ Loo, unasema, “Atauhukumu kwa Kristo.” Yeye ni Neno. Hawezi kuliondokea, linafunga moja kwa moja tena, Yeye ni Neno. Kwa hiyo sasa, kwa hiyo tunajua ya kwamba Neno hilo ni kweli. Na kama ukisema una Kristo wala huamini Neno hili, kuna kasoro na kile ulicho nacho, maana, Neno ni kweli, naam, bwana, haina budi kuwa ni Neno.

⁵⁹ Sasa, tunaona ya kwamba Mungu aliwapa watoto Wake kilicho bora zaidi, na kwa hiyo haimbidi kuliboresha. Yeye tu, habadiliki kamwe, hajabadilika hata kidogo tangu mara ya kwanza alipolitoa kwa ajili ya ulinzi wa watoto Wake. Sasa, alipojua... Kulikuwa na vita Mbinguni, ilimbidi kumfukuza Shetani, ndipo akashuka duniani na kuwakinga watoto Wake kwa Neno Lake.

⁶⁰ Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Wazieni tu, kwamba... Sasa, Hawa hakufanya hivyo, wakati alipokuwa amesimama katika Ngome hii kuu ya Neno Lake... Sasa, Shetani alikuwa nje akijaribu kutumia namna fulani ya mbinu kumwondoa Humo, kwa kuwa maadamu alikaa nyuma ya Neno, kila kitu kilikuwa sawa.

⁶¹ Hapo ndipo tunapofanyia kosa letu. Tunafanya kosa letu tunapoondoka nyuma ya Neno. Kwa hiyo ninaamini waaminio wote wa Biblia wanaliwazia hivyo. Tukiondoka nyuma ya Neno, basi tuko katika shida, bali maadamu tunaliweka Neno mbele yetu, usilitangulie Neno, acha Neno likutangulie, unaona, liache tu litangulie, nawe ishi tu papo hapo nyuma Yake. Linachimba shimo, nawe unatembea tu ndani yake. Unaona? Na hivyo ndivyo liendavyo.

⁶² Sasa, tunaona basi katika wakati huu mkuu wa—wa mwanzo, wakati Mungu alipowakinga watoto Wake katika Ngome hii ya Neno Lake, na—na kuwaambia, sasa hiyo ni, hiyo ilikuwa ndiyo... Sasa, wazia tu, Hawa hakukikataa tu Kitu hicho chote, hakusema, “Vema, Mungu, nadhani, amekosea kabisa. Siamini hata neno moja la hayo.” La. “Ninaamini nusu yake, Bwana.” Hapana. Shetani alieleza vibaya sehemu Yake ndogo tu, si lote, sehemu Yake ndogo tu.

⁶³ Na kwa sababu alisikiliza tamshi hilo moja dogo, imesababisha kila msafara wa mazishi, ikachimba kila kaburi, ikasababisha kila mvi, kila mtoto mchanga mgonjwa, kila dhambi iliyopata kutendwa, kwa sababu ya kuchukua tu chembe moja ndogo ya Neno la Mungu na kuliweka tu mahali pengine.

⁶⁴ Sasa, kama Mungu asiye na kikomo, Mungu aliyejaa upendo, kulielezea vibaya Neno Lake, kutoliamini lote, sehemu Yake tu, kungesababisha haya yote yatendeke kwa sababu ya kutokuliamini kidogo tu, ninaamini itatubidi kuchukua kila

sehemu Yake, turudi tena, kwa sababu kulipotosha tu, kusema, “Biblia inasema *hivi*, lakini kwa kweli haimaanishi hivyo.” Kweli inamaanisha hivyo. Mnaona? Inamaanisha hivyo jinsi *hiyo* tu. Kwa hiyo hatuna budi kuliweka hivyo, jinsi Yeye alivyolisema.

⁶⁵ Lakini basi Hawa angeninii...Sasa, tutaona mara tu yeye...Ilimbidi kupata, ilimbidi Shetani kuvutia usikivu wake. Sasa, mnakumbuka, yeye yuko katika vita na Mungu. Nao wanaume na wanawake ni watoto Wake, kwa hiyo Yeye yuko vitani na Shetani. Kwa hiyo sasa kumbukeni, Shetani hushuka kujita kutumia mbinu kujaribu kuvipinga vita vya Mungu, ulinzi Wake, anajaribu kupata kitu anachoweza, si—silaha bora zaidi. Kwa hiyo hakuna silaha bora zaidi ambayo angeweza kupata, kwa hiyo basi mbinu pekee angaliweza kutumia ingekuwa ni hoja. Loo, unaposimama kuhoji chochote!

“Neno linasema . . .”

“Lakini hebu nione, hilo halimaanishi mimi.”

“Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.”

“Hilo halisemi . . .” Linamaanisha hivyo pia. Hiyo ni kweli.

“Yeyote atakaye . . .”

“Vema, ninajua Roho Mtakatifu alikuwa kwa ajili yao huko nyuma katika siku za mwanzoni, lakini Yeye . . .Hoja tu zinatwambia kwamba sisi . . .” Loo, la, usifanye hivyo.

⁶⁶ “Yeyote atakaye, kwenu na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Mnaona? Mnaona? Hakuna hoja, usisimame kutoa hoja. Endelea tu kuamini, kuamini tu yale aliyosema.

⁶⁷ “Vema, Ndugu Branham, nimemtafuta Roho Mtakatifu kwa—kwa miaka kumi.” Unahoji nini? Kama ulitekeleza mpango Wake, basi endelea mbele tu, basi amini tu. Unaona? Aliweka mpango huo basi fuata tu mpango huo, ndipo haina budi kutokea vizuri. Kama sivyo, basi Yeye alisema uongo. Unaona? Kwa hiyo Yeye hawezi kutuambia chochote kibaya na bado awe Mungu. Kwa hiyo unaona, huna budi kuamini kwamba ni Neno Lake, la sivyo humwamini Yeye hata kidogo. Kwa hiyo—kwa hiyo ni ajabu, sivyo? Lakini ni kweli hasa, ni kweli hasa.

⁶⁸ Sasa, tunaona ya kwamba adui huyu mkuu wa Mungu aliwazia, “Sasa, mradi tu wataamini Neno hilo kamwe siwezi kuwafikia. Mradi tu maskini familia hiyo huko Edeni inashikilia nyuma ya Neno hilo, kamwe siwezi kuwagusa.” Wala hawezi leo hii. Hiyo ni kweli. Angali amezuliwa. Sawa. “Lakini kama ninaweza kutumia mbinu nzuri sana na kutoa hoja nzuri, nitoe hoja za kibinadamu, kwa sababu yeye ni mwanadamu, na kama ninaweza tu kutoa hoja za kibinadamu, basi tuta—tuta—tutashinda vita,” Shetani na Malaika zake. Lakini basi Hawa aliachilia.

⁶⁹ Kwa hiyo basi tunamjua adui yetu kwa mashambulizi yake. Labda hamkulipata vizuri, jinsi nilivyolisema. Tunamjua adui yetu: Wakati mtu yeyote, roho yeyote, mtu yeyote anapojaribu kutokukubaliana na Neno la Mungu, kumbukeni, huyo ni adui yako, huyo ni adui yako. Tunajua shambulizi lake la kale, hilo ndilo aliloivunjia jamii ya binadamu, na hivyo ndivyo anavyowavunja hata leo, na hivyo ndivyo anavyokuondoa kwa Mungu, ni kutokuliamini Neno Lake.

⁷⁰ Na njia pekee unayoweza kudumu katika ushirika pamoja na Mungu, na kuzungumza Naye wakati wa jua kupunga, ni kukaa umeimarishwa katika Neno pande zote mbili, uachilie pazia la Neno la Mungu likushukie pande zote, nawe uwe tone moja kwa moja katikati Yake. Hiyo ni kweli. Ndipo umeimarishwa. Utukufu!

⁷¹ Sasa, kusudi afanye jambo hili, hana budi kulifanya la kuvutia sana, kutoa hoja, na hivyo ndivyo Shetani afanyavyo. Yeye ni mzuri katika hiyo kazi, na ni adui mzuri. Naye huifanya ivutie, ilimbidi kuifanya imvutie Hawa, akasema, “Sasa, angalia, Mpenzi,” mnaona, “unajua, hujui mema na mabaya. Nawe hu—huna budi kukumbuka ya kwamba ni... tunda hili ni la kupendeza macho, li—li—litamfanya mtu awe na hekima, na yote...”

⁷² Loo, kama hicho si chambo kizuri! “Pata tu Ph.D. yako, ama LL., L. maradufu, Q.U., S.T.D.,” ama kitu kama hicho. “Utakuwa na hekima.” Kumbukeni sasa, hivyo sivyo ilivyo. Imani katika Mungu ndiyo inayofanya jambo hilo. Huenda ukawa na digrii za kutosha kuubandika ukuta *ule* na bado usimjue Mungu. Unaona? Unamjua Mungu kwa imani, si kitu kingine. Namna gani? Kwa imani. Nini? Imani katika Neno Lake; hiyo ndiyo njia pekee anavyoitambua imani. “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Hivyo ndivyo inavyokuja, kwa kusikia Neno la Mungu.

⁷³ Sasa, Shetani alilifanya livutie, angali analifanya livutie. Sasa, sidhalilishi chochote, natumaini hamtanielewa namna hiyo, mimi—mimi... kama ninafanya hivyo simaanishi hivyo. Lakini Shetani hujaribu kufanya theolojia na—na elimu kuvutia. Mbona, tumekuwa tukijaribu kuuelimisha ulimwengu kwa miaka elfu mbili, unazidi kuwa mbaya kuliko ulivyowahi kuwa. Mnaona? Huwezi kuwaleta watu kwa Kristo kwa elimu, kwa madhehebu, wanajaribu kulifanya la kupendeza. Dhambi inapendeza, bila shaka, inapendeza.

⁷⁴ Sasa, kama ukichukua katika Biblia, tunaona... Nilikuwa nikizungumza hapa, siku chache zilizopita usiku mahali fulani juu ya somo la Nuhu katika siku zake. Chukueni Mwanzo 6, wakati “wana wa Mungu walipowaona binti za wanadamu.” Basi wakati mmoja nilikuwa nikisoma historia na nilikuwa nikisikiliza vile mwanahistoria alivyokuwa akitoa ninii yake,

ama, la, samahani, ilikuwa ni maelezo juu ya kile alichodhania wa—wale “wana wa Mungu” walichokuwa, akasema ilikuwa ni Malaika walioanguka wakajisukumiza katika miili ya wanadamu na kuwaona wanawake, na jinsi wanawake walivyovutia, ndipo wana hawa wa Mungu wakafanyika mwili.

⁷⁵ “Kama ukilichukua hivyo,” niliwazia, “ndugu yangu wa thamani, wewe ni mwerevu kuliko mimi, lakini ukifanya hivyo, unamfanya ibilisi muumba basi.” Kwa hiyo ibilisi hawezi kuumba, yeye hupotosha tu kile Mungu alichoumba, kuna Uumbaji mmoja tu, huo ni Mungu, Muumba mmoja. Kosa ni haki iliyopotoshwa, uongo ni kweli iliyotumiwa vibaya, mnaona, uzini ni tendo sahihi likitumiwa vibaya, mnaona. Makosa yote ni haki iliyopotoshwa. Na hayo tu ndiyo Shetani anayoweza kufanya, ni kupotosha tu yale Mungu amefanya tayari, mnaona, upotovu. Vema.

⁷⁶ Sasa, tunaona ya kwamba mara nyingi Shetani hulifanya la—la kuvutia sana, upate kuwa maarufu zaidi. Sasa, hivyo ndivyo alivyomfanyia Hawa, mwenye hekima, mwerevu, tajiri. Siku hizi amelifanya la kuvutia sana hata watu wanataka kuweka mamilioni ya dola katika majengo, na kisha kuhubiri ati Kuja kwa Bwana kumekaribia. Unaona?

⁷⁷ Makanisa yanajenga kumbi kubwa zaidi, na—na kununua mashamba zaidi na—na kila kitu, na halafu kuhubiri Kuja kwa Bwana kumekaribia, huku wamishenari wakiwa hudumani wakijaribu kulipeleka Neno kwa watu maskini ambao hawakuwa wamelisikia hata wakati mmoja, na inawabidi kuteseka kwa ajili yake, mnaona. Halionekani kuwa sawa, kwangu mimi. Lakini Shetani anajaribu kulifanya la kuvutia, anayatengeneza makanisa, analifanya kanisa la kiakili, zuri, lenye akili.

⁷⁸ Ninaishi karibu na—na dhehebu *fulani*, ni watu wazuri, wazuri sana, nadhani, na hao watu. Lakini mzee mmoja, ameketi nje akijaribu, akingojea kuombewa, na kwa sababu mhudumu huyu hakuamini katika kuwaombea wagonjwa, sikuwa mahali hapo wakati huo, mzee huyo alikuwa akingojea, akivamia, akipuliza, na kwa sababu mzee huyo kwa namna fulani, alionekana kama mzururaji, maskini mzee huyo hakuwa na viatu vizuri miguuni mwake, nalo koti lake kuukuu lilikuwa limechakaa na limechanika, na, lakini mhudumu huyu hakuninii. . . hata hangemruhusu aje barazani, atoke kwenye mvua. Nami nilishangaa tu kama, tutakapofika Mbinguni, kama kutakuwa tu na mahali maalum, padogo pa wenye elimu, huku maskini na kadhaliika wakiwa mahali pengine.

⁷⁹ Sasa, ninahofu kutakuwa na masikitiko mengi sana kwenye Hukumu, kwa sababu mnajua, Paulo alisema katika Waebrania mlango wa 11, “Walizunguka-zunguka wamevaa ngozi za

kondoo na ngozi za mbuzi, walikuwa wahitaji, na wanaoteseka.” Mwangalie Eliya pangoni mwake, na jinsi ambavyo kama tungemwona akija mlangoni petu leo, amejaa ndevu usoni mwake, kichwa chake chenye upara kiking’aa, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, labda tungemfukuza uani, baadhi ya ndugu zetu wasomi. Hiyo ni kweli.

⁸⁰ Lakini hujui ni kitu gani kinachopigapiga chini ya maskini ngozi hiyo ya kale hapo. Mnaona? Huenda Roho Mtakatifu amefanya maskani humo. Mnaona? Hatupaswi kamwe kufanya hivyo, hatuna budi kuwa ndugu, kumtendea mwanadamu, haidhuru kama yuko makosani, bado mtendee mema, uwe mwema kwake. Kama huna Roho huyo, basi kuna kasoro. Yesu alikuwa mwema kwa wale waliokuwa wabaya Kwake, mnaona. Hamna budi kuwa Wakristo, waliojaa upendo, tayari kusaidia jamii yoyote, rangi, kanuni za imani, mahali popote, wakati wowote. Mnaona? Hatuna budi kuwa hivyo, hao ni Wakristo, hivyo ndivyo Kristo angetutaka. Na kuwa Mkristo ni kuwa kama Kristo.

⁸¹ Sasa, Shetani akifanya kila kitu kuvutia sana hata hivyo, na kuweka watu kando, na, “Lazima uamini kanuni *hii* ya imani na hilo tu ndilo unalopaswa kufanya.” Na, “Huna budi kuyakariri maombi *haya*, na kukata mambo,” na kadhalika. Inaonekana kama . . . Huku watu wanaendelea kuishi, wangali wanacheza kamari, wanavuta sigara, wanakunywa pombe, wanawake wanavaa nguo za kizinifu, na—na wanaenda kwenye maonyesho, madansi, na kucheza karata, kama tu walivyofanya daima. Mnaona? Lakini hata hivyo wao ni wa kundi kubwa, la juu, la watu wenye akili. Mnaona, Shetani hulifanya la kuvutia sana; hilo silo.

⁸² Je, mliiona ile dhabihu ya Kaini, jinsi ilivyoonekana ya kuvutia, ya kupendeza, matunda ya kondeni pamoja na maua? Lakini ya Habili haikuwa ya kuvutia, huku akimvuta maskini mwana-kondoo kwa kipande cha, sidhani walikuwa na katani siku hizo, huenda ilikuwa ni mzabibu uliozungushiwa shingoni mwake, naye akampeleka kule juu na kukata maskini koo lake kwa mwamba mpaka akatokwa na damu hata kufa, haikuwa ya kuvutia sana, bali ilikuwa haki ikijibia dhambi.

⁸³ Lakini Mungu hulifanya tu Neno Lake halisi zaidi wakati wote. Haimbidi kuliimarisha tena, na kuinua kitu kingine, Yeye hulifanya tu Neno Lake halisi zaidi wakati wote. Nayo Biblia ilisema, “A—adi anapokuja kama mafuriko, Roho wa Mungu huinua beramu dhidi yake.” Mnaona? Sasa, ni nini . . . ? Basi kama adui akija kama mafuriko, na Ngome ya Mungu ya kuwakinga watu Wake ni Neno la Mungu, kwa hiyo Yeye huinua tu Neno, Beramu dhidi yake. Amina.

⁸⁴ Sasa, Yeye ameiinua mara tatu. Mlijua nini? Mungu daima yuko katika tatu. Usininii . . . Hiyo ndiyo namba kamilifu ya

Mungu. Kama vile Mungu, Kiini chenyewe cha upendo, Roho hufunika mifumo yote ya jua, kutoka Umilele, kama kulikuwako na njia kama hiyo, hadi Umilele, upendo wote, nguvu zote, nguvu halisi. Sasa, upendo huo hapo si wa *fileo*, neno la Kiyunani linauweka katika upendo, bali, upendo wa ushirika, bali ni *Agapao*, upendo wa kiungu, Naye ndiye Chemchemi ya hayo yote.

⁸⁵ Na sasa wakati hayo yote. . . Yeye aliwatia mafuta manabii, watu waliozaliwa kwa kujuana kimwili, bali isingefaa kitu. Sasa, wakati mmoja basi Mungu alifanyika mwanadamu, naye Yesu alikuwa ndiye Mtu huyo, Naye alikuwa ndiye Sura iliyodhihirishwa ya Baba, mnaona. Kwa maneno mengine usafi huu wote mkuu wa upendo, usafi mkuu wa nguvu, kitu hiki chote kikuu kilidhihirishwa ndani Yake. Sasa basi, Yeye alishuka kwenda kaburini na akafa kwa ajili yetu kwa ajili ya utakaso wetu na kuhesabiwa haki, na kisha anamrudisha Roho Mtakatifu, mnaona, kwa ajili yetu. Sasa, basi, sisi tumehesabiwa haki, Kristo alikuwa ndiye utakaso wa Mungu, sisi ndio kuhesabiwa haki, Kristo utakaso, naye Baba, Kichwa. Mnaona?

⁸⁶ Kama tu vile, Neno hapo mwanzo lilinenwa kwetu katika bustani ya Edeni, Neno lililonenwa, ndipo mara ya pili likafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, na mara ya tatu likafanyika sehemu yetu katika Roho Mtakatifu, akikaa ndani yetu, Mungu akiingia ndani ya mwanadamu. Kwanza alinena Neno, adui akalirarulia mbali; ndipo akafanyika mwili, akasulubiwa; lakini sasa, amina, kuna tofauti katika Neno, Neno limekuwa Kanisa, nalo Kanisa ni Neno, Mungu. Yote aliyokuwa Mungu aliyamimina ndani ya Kristo, yote aliyokuwa Kristo, aliyamimina ndani ya Kanisa, Roho Mtakatifu. Sasa, adui ana kitu fulani, mnaona, basi hapigani na kitu fulani *hapa* nyuma.

⁸⁷ Watu wengi wamechukua tu andiko, “Andiko huua, Roho huleta Uzima,” mnaona. Mnaona? Nao wanachukua kanuni hizi za imani na kadhalika, zingali zinaua, bali wakati unapomchukua Roho, huyo ni Mungu, Mwenyewe. Unajuaje ni Mungu? Kwa sababu Yeye analichukua Neno na kulidhihirisha. Unaona? Basi ni Mungu, Mwenyewe. Loo, jamani! Neno Lililonenwa. Naam, bwana.

⁸⁸ Loo, jamani! Ninawazia huko nyuma katika siku za Nuhu, Yesu alizilinganisha na siku hizi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. . .” Mwanzo 6. Nitalifikia Andiko hilo tena papa hapa. Hivi mliona, wakati wana wa Mungu. . . ambao walikuwa wana wa Sethi waliotokana na Adamu, na kutoka kwa Adamu alikuwa Mungu, mwana wa Mungu, mwana wa Sethi, ndipo upande wa pili ulitoka kwa Kaini, ambao ulikuwa ukiamini uongo wa Shetani, wana wa Shetani.

⁸⁹ Sasa, wakati hao wanawake Wakanaani, moja kwa moja kwenye wakati wa mwisho kabla ya yale maangamizi, walikuwa

warembo sana. Mmeona tofauti katika sura za wanawake, baadhi yenu wanaume na wanawake wa umri mkubwa zaidi, kwa miaka michache iliyopita?

⁹⁰ Nilikuwa nikisoma hivi majuzi ambapo Pearl White, wengi wenu wazee mnakumbuka, mmoja wa wanawake warembo sana taifa hili lilikuwa nao, na wakati Scott Jackson alipomdunga kisu akafa, mpenzi wake mnyamavu, mpenzi wa siri, hasa, nayo picha yake, mbona, asingeweza kusimama mtaani na chochote kinachoonekana kirembo siku hizi. Lakini mnaona, tunakaribia mwisho, nao wanawake wanajigeuza katika va—vazi linalowafanya. . . Mnaona? Huyo ni Mkanaani. Afadhali nisisame papo hapo na kusogea *hapa* sasa, mnaona, maana nilisema nisingesema hilo tena.

⁹¹ Vema, Shetani ana majitu wake wa kielimu, mnakumbuka walisema kulikuwa na majitu nchini siku hizo, majitu, angali anao, majitu wa kielimu. Loo, jamani! Mnaona? Katika siku hizo wakati Nuhu aliponena kuhusu, “Kunakuja gharika,” mnaona, wao hawakuamini hilo, hata hivyo walikuwa wa kidini, bali wao. . . haikukubaliana na maelezo yao ya sayansi, jinsi ambavyo itanyesha huko chini, wakati hakuna mvua huko juu, ilithibitishwa kwa sayansi, hakuna mvua huko juu.

⁹² Kama yule jamaa wa Kirusi, hivi majuzi katika mzingo huo, alisema ya kwamba aliruka kila mahali kule, mara kumi na saba kote ulimwenguni, hakumwona Mungu, wala Roho Mtakatifu, wala Malaika. Maskini mtu mjinga. Naam. Hilo ni jambo lile lile, sayansi yao, ni ninii tu, wa—wa—wanakuwa wa kisayansi sana wanakuwa bubu, mnaona, ama—ama, samahani, sikupaswa kusema hivyo, ni—ninamaanisha wanapuza tu mambo yaliyo halisi, mnaona.

⁹³ Sasa, vema. Lakini leo hii, Shetani ana majitu wake wa kielimu, wanaweza kuelezea kila sehemu yake vinginevyo. Hakika. “Hakuna upuuzi kama huo. Aa, kuna. . . Ati uponyaji wa Kiungu? Aa, wendawazimu.” Mnaona?

⁹⁴ Roho wa Bwana kuninii. . . Biblia ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili,” Waebrania, mlango wa 4, “kali kuliko upanga ukatao kuwili, unakata hata kwenye mafuta ya mfupa, na ninii. . . na hata M—Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo.” Roho huyo wa Mungu, wakati Yesu aliposimama na kutambua kile walichokuwa wakiwazia, wakati Yeye alipokuwa. . . Yeye alikuwa ni Neno.

⁹⁵ Wakati Filipino alipomjia na—na kumleta Nathanaeli, Alisema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!”

Kasema, “Rabi, ulipata kuniona lini?”

⁹⁶ Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Whiu! Hmm! Hiyo ilikuwa ni nini? Hilo lilikuwa ni Neno. Neno, lenye ukali zaidi, kali zaidi!

97 Wakati yule mwanamke kisimani alipokuja na kusema, wakati alipoomba maji ya kunywa naye mwanamke akasema, “Mbona, si kawaida, kuna ubaguzi hapa. Sisi...Ninyi ni Wayahudi nasi ni Wasamaria.”

“Lakini,” Yeye akasema, “kama ungejua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.”

Ndipo mazungumzo yakaendelea mpaka alipoona, Neno hilo lilianza kupata mahali Pake. Kasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Kasema, “Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si wako.”

98 Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ndiwe Mtiwa Mafuta, yule Kristo, naona kwamba Wewe ni nabii,” akasema. “Nasi tunajua wakati yule Aliyetiwa Mafuta atakapokuja,” atakuwa ni Neno, “Yeye atatwambia mambo haya.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Mnaona? Mnaona? Huyo hapo Neno. Loo, hilo Neno, jamani! Hmm! Naam, bwana. Vema.

99 Sasa, mnaona, Neno si lazima lithibitishwe kisayansi maadamu ni Neno. Kama linaweza kuthibitishwa kisayansi, basi inawezekana kwamba si Neno. Unasema, “Kama halijathibitishwa kisayansi, si kweli.” Basi kama una akili, unaamini una akili? Basi nithibitishie kisayansi unayo.

100 Je, unapenda? Ni wangapi wanaopenda? Vema, sijui kama ningeweza kununua kidogo kwenye duka la dawa, ninahitaji mwingi sana. Huh? Upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, utu wema, subira, na imani, mambo hayo ni...hayawezi kuthibitishwa kisayansi, na ndiyo mambo ya kudumu pekee tuliyo nayo. Hiyo ni kweli. Hakuna kitu kinachodumu ila hicho, unaona, na hakijathibitishwa kisayansi. Vema.

101 Sasa, lakini siku hizi...katika wakati wa Nuhu walikuwa na hao majitu mashuhuri, na leo hii wana hao majitu mashuhuri wa kielimu nchini pia. Hiyo ni kweli. Basi, nachukia kusema hivi, kama—kama kuna mmoja hapa, natumaini sikuudhi, bali ni wapelelezi wa Shetani tena. Ati nini? Hakika, majitu wa kielimu wanakuja kuthibitisha ya kwamba kupiga makelele huku kwote na kusema, “Amina,” na kwenda madhabahuni, na kuvunjika kwa sababu ya dhambi zako, ya kwamba hayo yote ni mhemuko tu.

102 Mnaona, hilo ni jitu la kisayansi, hilo ni jitu la kielimu, “Hakuna kitu kama hicho.” Anatembea huku mwenye macho makavu, na loo, anasema tu, “Vema, nitajiunga na kanisa hili, nami...” Loo, jamani! “Vema, ninaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.” Shetani anaamini pia, sio ishara kwamba ameokoka. Mnaona? Inahitaji zaidi ya hayo, inahitaji kuzaliwa

upya. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli. Kwa hiyo inahitaji, unaona, Neno, inahitaji kuzaliwa upya, sio tu kusema hivyo, inahitaji jambo fulani linalotukia *hapa* ndani, na kukufanya tofauti.

¹⁰³ Na jinsi tulivyo na furaha, usiku wa leo, kwamba tumelipata! Ni wangapi wamefurahi kwamba mmezaliwa upya? Loo, nina furaha sana! Hebu tupige hatua kidogo. Ninasema mambo mengi, kama tu mtu mwingine yeyote, mwajua, ninachanganyikiwa kabisa na kila kitu, lakini mara moja moja Bwana hunipa kitu fulani na—nami, vema, na—nalipenda sana, lakini . . . Nanyi mnajua, nikisoma, kila wakati ninaposoma Neno Lake, daima ninafanya hivyo, kwa sababu Hilo ni kamilifu. Lakini wakati mwingine Yeye hunijalia kusema jambo fulani, mwajua, linasikika zuri sana kwangu, na Yeye aliniruhusu kusema jambo fulani hivi majuzi, lilinisaidia sana. Loo, jamani! Linasikika la kindani sana, endapo si la kupinga dini, ama, halifai kusemwa.

¹⁰⁴ Nitawaambia ilikuwa ni nini, nilikuwa nikiwazia juu ya dhamana yetu. Tunajuaje, kuna mambo mengi sana mbalimbali, tunajuaje uko sahihi? Dini nyingi sana ulimwenguni na kadhalika. Tazama, wakati mmoja Israeli walikuwa huko chini Misri, na kama watu wa Mungu, walikuwa wamekaa huko chini kwa mamia ya miaka, nao walikuwa ni watumwa, wakisukumwa huku na huku vyovyote. Naye adui angetokea, na kikapu kilichojaa mikate ya siku nyingi, iliyoota kuvu na kuitupa, iliwabidi kuila, wafe. Nao binti zao wadogo walibakwa, hakuna kitu wangaliweza kufanya kulihusu, hakuna kitu. Wakitaka kumwua mwana wao, walimwua tu, hivyo tu. Lilikuwa ni jambo la kuchukiza jinsi gani!

¹⁰⁵ Kwa hiyo akishuka kutoka nyikani akaja nabii akiwa na Nguzo ya Moto, walisema, iliyomfuata. Alikuwa anakuja kuwaletea ujumbe kwamba “Kuna nchi ambayo Mungu anayo kwa ajili yenu.” Nao wakamsikiliza nabii huyu.

¹⁰⁶ Kutoka . . . Misri wakaenda, kwa mkono wa Mungu, wakafika mahali paitwapo Kadeshi-barnea. Kadeshi-barnea ilikuwa ndiyo kiti cha hukumu, kiti kikuu cha hukumu, wakati mmoja, cha ulimwengu, naambiwa. Na hapo walikuwa na mmoja miongoni mwao, shujaa mkuu, jina lake Yoshua. Ninaamini linamaanisha “Yehova-Mwokozi.” “Yehova-Mwokozi,” *Yoshua*. Shujaa huyu mkuu, mnajua alilofanya? Alitaka kuwaonyesha watoto kwamba hiyo . . .

¹⁰⁷ Mnaona, hakuna hata mmoja wao aliyewahi kuwa huko, hawakujua kweli kwamba nchi hiyo ilikuwako, waliamini tu. Jambo ndilo hilo, jambo ndilo hilo. Kile tu . . . Nabii huyu aliwaletea Neno la Bwana, bila shaka Neno huja kwa njia ya manabii, mnaona. Kwa hiyo basi wao, kwa hiyo wakaja . . . Nalo Neno la Bwana lilimjia nabii huyu, naye akawaletea na kusema, “Kuna nchi iliyojaa maziwa na asali ambamo mnaweza kuwa na

mashamba yenu wenyewe, kuwalea watoto wenu na kuwalisha, na kuishi kwa amani.”

¹⁰⁸ Kwa hiyo Yoshua alipokaribia kule kwenye ile hukumu, ile Kadeshi-barnea kuu. . . Nasi sote tunajua hadithi hiyo, hapo ndipo Israeli ilipata hukumu yake pia. Kwa hiyo basi Yoshua akavuka Yordani, akaingia kwenye nchi ya ahadi, na akarudi na ushahidi kwamba hiyo nchi ilikuwa halisi, alikuwa na zabibu, alikuwa na zabibu ambazo wangeweza kuzionja, kwamba hiyo nchi ilikuwa halisi, ungeweza kunyosha mkono na kuonja za—zabibu. Mbona, zilikuwa kubwa sana hata watu wawili walibeba kichala chake begani mwao. “Loo,” akasema, “hiyo nchi ni halisi.”

¹⁰⁹ Kwa hiyo hao watu wakavuka, wakajenga makazi yao, walikuwa na taifa lao wenyewe, waliishi kwa amani, Mkono wa Mungu ulikuwa juu yao na kuwabariki, na kuwapa watu wenye nguvu. Na kuwazia. . . Lakini baada ya kitambo kidogo, walipozeeka, hatimaye walishuka wakafa. Ndipo wangekufa, na muda si muda mwajua, ubavuni mwa vilima kukaanza kufunikwa na makaburi, makaburi ya wenye haki, manabii, na—na wenye hekima na wafalme, na—na watu wenye haki.

¹¹⁰ Kwa hiyo basi kule, Shujaa mwingine mkuu akashuka, loo, Yeye alikuwa ndiye Mfalme wa hao wote, aliitwa, Mfaransa anamwita “Jésus,” Yesu, Shujaa, Yehova. Naye akashuka Naye aliwapenda, bali Yeye akasema, “Mnajua hamna budi kuzeeka na kufa, bali kuna Uzima baada ya mauti, Uzima baada ya mauti. Kwa maana katika Nyumba ya Baba Yangu mna makao mengi, kama sivyo, ningaliwaambia.” Mnaona, Yeye anafanya nini? Anatwambia sisi wazee ya kwamba kuna Nchi, baada ya sisi kupitia humu, kuna Nchi nyingine. Sio kwamba tu alikuwa na Nguzo ya Moto iliyomfuata, Yeye *alikuwa* ndiye hiyo Nguzo ya Moto, ninaamini, mnaona, mnaona, Yeye alikuwa, yule Malaika wa Agano.

¹¹¹ Kwa hiyo Huyu hapa, Naye akasema, “Baada ya mtu kumalizia hapa nawe umekamilisha wakati wako, huu ni wakati wa mbegu, lakini kuna Nchi ng’ambo ya hii anayoishi mwanadamu.” Akafikia Kadeshi-barnea Yake, inaitwa Kalvari. Hapo si kwamba tu. . . alihukumiwa, bali alihukumiwa kwa ajili yangu na yako, akazichukua dhambi za Adamu. Na hapo akaistahimili ile hukumu, akavuka mto Yordani, wa mauti, lakini katika siku ya tatu akarudi. Yeye alikuwa nini? Akileta ushahidi, kama Yoshua, alileta ushahidi ya kwamba Nchi hiyo ni halisi, ya kwamba mtu huishi baada ya kufa. Haleluya! Mwanadamu huishi baada ya kufa.

¹¹² Ayubu alisema katika Ayubu 14, “Mtu akifa, je, anaweza kuishi tena, au, ataishi tena? Siku zote za wakati wangu ulioamriwa nitangojea, hata badiliko langu litakapokuja. Najua Mkombozi wangu yu hai.” Akiwa nabii, mamia ya miaka

kabla...Wakati Elihu alipozungumza naye na—na Roho wa Mungu akamjia nabii huyu, aliyejaa majipu, na katika hali mbaya sana, alikuwa amepoteza kila kitu alichokuwa nacho ila uhai wake, naye alikuwa ameketi pale, wakati Roho alipomshukia, akaangalia chini kupitia mkondo wa wakati kwa miaka elfu nne, naye akaona kule Kuja kwa Bwana, akasema, “Najua Mkombozi wangu yu hai, katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu ya ngozi yanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, Ambaye nitamwona mwenyewe, macho yangu yatamwona, na si mwingine.”

¹¹³ Naye hapa akavuka Yordani baada ya kusimama hukumuni kwa ajili ya ulimwengu. Naye akavuka Yordani, akarudi, baadhi yao wakasema, “Ni roho.”

Kasema, “Nishikeni. Je, roho ina mifupa na nyama kama niliyo nayo? Na jambo lingine,” Yeye anasema, “mna chakula?” Mnaona?

“Naam.” Nao wakampa samaki na mkate, Naye akala.

Akasema, “Sasa, roho haili namna hii.” Amina.

¹¹⁴ Lakini Yeye akasema, “Enyi watoto, tokeni hapa nje mkabatizwe katika Jina Langu sasa, ninawatakeni mkiri dhambi zenu. Kisha mwende mkangojee huko juu kwenye mji wa Yerusalemu, nami nitawapa Arabuni ya Huko.” Hmm! “Nitawapa Arabuni ya wokovu wenu.” Mnajua arabuni ni nini, ni malipo ya kwanza, ni—ni baadhi yake, ni kidogo tu cha—cha kilicho halisi. “Sasa, nitawapa Arabuni yake.” Ndipo wakangojeka mpaka siku hiyo ilipokuja, nao wakapokea Arabuni ya wokovu wao.

¹¹⁵ Sasa, wazieni hilo enyi marafiki, hakuna tena...Tunaenda zetu. Wapi? Kwenye Nchi ya ahadi, tunasafiri. Pamoja na Nini? Ushahidi. Yoshua wetu amerudi, utukufu, nasi tunao Ushahidi. Kwa kuwa wakati mmoja tulikuwa katika dhambi na makosa, lakini tukayafia mambo ya ulimwengu, nasi tumezikwa ndani Yake na kufufuka pamoja Naye katika kufufuka Kwake. Na sasa, tuko juu juu ya mambo hayo, tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

¹¹⁶ Tunaishi, ule Ushahidi. Unajuaje Yeye yu hai? Vema, ninaishi juu ya hayo, tayari nimeinuliwa kutoka kwenye hayo, tayari nimeonja malimbuko ya ufufuo. Jambo ndilo hilo, hilo ndilo ninalozungumzia.

¹¹⁷ Sasa, naam, bwana, wale wapelelezi wakaingia, hawa wapelelezi wa kielimu kupeleleza, nao wakaona mahali kitu fulani kinapoanzia hapa, ndipo wakakielekezea bunduki zake, na kuwafanya wanawake wote waanze kuvalia kiovu, wanawafanya wanaume wote waanze kuchukua na kusema uongo. Loo, anaweza tu kuwamwagilia, mnaona, maana wao ni

majitu halisi. Lakini mnajua, hilo limezidi sana kwa maskini watoto wa Mungu, wanyenyekevu. Naam, hiyo ni kweli.

¹¹⁸ Mnajua, na watu hawa wananyemelea, wakiwapotosha. Mnajua Yuda alisema, katika Kitabu cha Yuda, yeye alisema, “Wananyemelea kisiri, wanaingia kisiri, watu wa kale waliokusudiwa tangu zamani hukumu hii.” Huamini jambo hilo, na hilo je? Naam. “Waliokusudiwa tangu zamani hukumu hii.” Ati nini? Wakaingia, hawa majitu wa kielimu wakiingia, wakinyemelea, “wabadilio neema ya Mungu kuwa ufisadi,” mnaona, “kuigeuza imani ya watu.” Loo, jamani!

¹¹⁹ Wanafanya nini? Wanafanya nini wanapoingia? Wao, wakijaribu kuwafanya. . . Wao ni wapelelezi wa Shetani, wakiwaambia, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu.” Loo, wamekuja wamechelewa sana kwa jambo hilo, tunajua vizuri zaidi. Naam, naitakia heri maskini mioyo yenu, tunajua vizuri zaidi. Naam, bwana.

¹²⁰ Lakini wanafanya nini? Wanajaribu kuwafanya, kama tu Shetani alivyofanya, kupoteza imani yenu katika Neno. Wanajaribu kusema, “Siku za miujiza zimepita. Huko ni kuchochewa tu kiakili. Hakuna kitu kwake, na mambo haya yote hapa,” kujaribu kuelezea utukufu wote vibaya, mema yote vibaya. “Loo, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Mungu haukusudii.”

¹²¹ Sikiliza ndugu, nitakuonyesha, nawe unaweza kunionyesha, ambapo Mungu aliliahidi Kanisa, nami, kile ninachotaka ufanye, ni kunionyesha mahali alipoliondoa Kwake. La, la. Sasa, Yeye hafanyi hivyo, la, kama kuna lingine, Yeye anaongeza zaidi kidogo kwake. Unaona? Yeye haliondoi, Yeye huliongezea tu, kama alivyolifanyia Neno Lake. Yeye alisema Neno Lake, hivyo tu. Kwamba Yeye. . .

¹²² Na kama Agano la *Kale*, agano la *kale*, ule upatanisho wa *kale* ulikuwa na uponyaji ndani yake, ni zaidi sana vipi hili lililo bora zaidi? Hakika. Lina zaidi ya uponyaji, lina uponyaji wa nafsi, mwili, akili, roho, kila kitu. Ninii. . . Hakika ndivyo, lina Uzima wa Milele ndani yake, hakika linao, kwa sababu ni Uzima wa Mungu ukidhihirishwa katika Neno Lake kwa kuliadini.

¹²³ Sasa, lakini wananyemelea ndani kisiri, vema, na kujaribu kuiharibu imani yako. Wanajaribu tu kuiondoa, unaona, kwa hoja zao zilizoboreshwa za seminari, mwajua, wanaingia na kutoa hoja, “Sasa, angalia hapa, si ni *wazi sasa*?” Mngeweza tu kuwazia katika siku za Yesu wangepanya jambo lile lile? Wanakuja na kusema, “Sasa, si ni jambo la busara. . .?”

¹²⁴ Ninaweza kuwazia. . . Daima nimejaribu kuigiza, nikiwazia juu ya—juu ya Filipo wakati alipokuja pamoja na Nathanaeli. Naye Nathanaeli akasema, “Sasa, hebu tusemezane, Filipo. Sasa, kama, unajua kama Masihi angekuja, Yeye angeshuka moja kwa moja kwenye ushoroba wa Mbinguni na angeninii. . .

unajua kile Yeye angefanya? Angeshuka aende moja kwa moja kwenye ua wa hekalu ambao Musa aliweka wakfu.” Huo ulikuwa ni wakati wa Musa. Hiyo ni kweli. “Naye angekuwa huko juu, naye Kayafa kuhani wetu mkuu angejua yote kuhusu hilo, unaona, hiyo ni kutoa hoja tu.”

¹²⁵ Lakini Yeye alikuwaje? Sio kushuka kupitia ushoroba wa Mbinguni, bali kupanda ukingo wa Yordani wenye matope; si kwa Kayafa, bali m—mhubiri aliyejaa mandevu alikuja pale amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, alikuwa tu akiyakemea hayo madhehebu ya siku hizo, kuyararua vipande-vipande, kasema, “Enyi uzao wa nyoka nyasini, ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo?” Ni tofauti jinsi gani! Lakini jinsi hasa Yeye alivyosema angekuja, bali walilifasiri vinginevyo. Mnaona hilo? Majitu wao wa kielimu walikuwa wakiwasomea, mnaona. Huna budi tu kumwacha Mungu akusomee Hilo. Roho Mtakatifu aliliandika Neno, kwa hiyo Roho Mtakatifu hulifasiri Neno...?...

¹²⁶ Sasa, vema. Walijaribu katika siku zao kumjaribu Nuhu asiamini Neno la Mungu. Ninaweza kumwona Nuhu akiingia katika safina hiyo, mwajua. Alihubiri, akasema, “Mvua inakuja, hakuna lingine. Inashuka.”

¹²⁷ Jitu likasema, “Loo, jamani! Usimjali huyo mzee mpumbavu. Mbona, a—amerukwa na akili. Unaona?” Lakini akaendelea mbele, na miaka mia moja na ishirini akaijenga safina hii.

¹²⁸ Sasa, ninaweza tu kuwazia nikiona, baada ya Mungu kusema, “Vema, Nuhu, nimesikia machukizo yao ya mwisho kutoka kwao nitakayovumilia. Kwea uingie safinani.” Naye Nuhu akaangalia wakiingia mle, na hapo wakaenda simba, chui, wawili-wawili.

¹²⁹ Ninaweza kusikia ninii, watu wote wakisema, “Panda juu kule, ewe mtakatifu anayejibingirisha, pamoja na wanyama wako wanaovunda,” mnaona. Wakipiga makelele, “Panda uende huko juu pamoja na maskini wanyama hao wanaovunda, ukitaka.” Lakini mnajua, yeye hakukaa na wanyama wanaonuka, aliendelea tu kupanda juu mpaka akafika juu, mnaona, ndipo Mungu akafunga mlango.

¹³⁰ Halafu mnajua nini? Nuhu alijaribiwa imani yake. Naam, alijaribiwa, mnaona, maana, mwajua, aliingia mle tarehe kumi na saba Februari, lakini mnajua nini? Haikunyesha kwa siku saba. Siku ya kwanza ikapita.

¹³¹ Ninawazia baadhi ya waaminio wakwamia mpakani walikuja na kusema, “Vema, unajua, mzee huyo huenda alikuwa sahihi. Mwajua, huenda kukawa na kitu fulani huko juu ambacho hata hatuwezi kukiona, labda sayansi haikuchuguza juu sana vya kutosha, kwa hiyo huenda tukaninii, tutapanda

juu tukasimame huko karibu, tukae tu mkutanoni kwa muda kidogo tuone kitakachotukia.”

¹³² Loo, jamani! Halijabadilika, hata kidogo, mnaona. Wanataka tu kupata kosa moja, na hakika ilionekana kana kwamba walilipata, maana siku ya kwanza walipokuja, kasema, “Vema, tutapanda huko juu, na kama ndivyo ilivyo, tutamwita Papa Nuhu, na kumwambia ashuke, ashushe ngazi ya kutuchukua.” Kwa hiyo wote wakakaribia, waaminio wakwamia mpakani, hao wengine wakaendelea kusababisha mafarakano na kucheka.

¹³³ Hao wengine, kwa namna fulani walikaa karibu, wakamsikiliza Nuhu mara moja moja, kasema, “Huenda ikawa ni kweli, kwa hiyo tutasimama hapa karibu, hata kama mlango umefungwa, tunaweza kuingia, Nuhu ana moyo mzuri, ataturuhusu kuingia.” Lakini mnajua, Mungu aliufunga huo mlango, Nuhu hakuwa na uhusiano wowote nao.

¹³⁴ Ndipo basi muda si muda mwajua, siku ya kwanza, Nuhu akasema, “Ninyi nyote jiwekeni tayari sasa, enyi watoto wote jiwekeni tayari sasa, mtasikia sauti ya kitu fulani, na itakuwa ni kitu msichojua chochote juu yake. Hamjawahi kusikia kelele kama hiyo, itakuwa mbaya kuliko mlipuko. Nayo itashuka kutoka angani, na giza kuu, nililionga katika ono, nayo maji yatabubujika huko nje kama chemchemi.”

Siku ya kwanza jua likachomoza, na, kasema, “Aisee.” Saa nne, saa sita, saa tisa, saa kumi na moja, hakuna mvua. Nuhu akawazia, “Ngoja kidogo.”

Wote wakasema, “Aa, hakukuwa na chochote kwake. Vema, hebu tujaribu siku nyingine.”

¹³⁵ Siku ya pili: “Itakuwa hapa asubuhi. Imechelewa kidogo, hiyo ni sawa, itakuwa hapa.” Na kesho yake asubuhi, saa tatu, saa nne, saa tano, hakuna mvua. Siku tano zikapita, siku sita zikapita, ilibidi atoe jasho.

¹³⁶ Hiyo ni kweli, hatuna budi kutoa jasho pia. Uh-huh. Lakini kama Mungu alisema jambo lolote, dumu nalo. Ni, “Kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.” Nasi tunalichukua Neno Lake, tunalitolea jasho. Mungu aliahidi Roho Mtakatifu, iweni kama mzee Buddy Robinson, kasema, “Bwana, usiponipa Roho Mtakatifu, utakaporudi utakuta lundo la mifupa limewekwa papa hapa.” Jambo ndilo hilo, litolee jasho, kaa hapo, “Mungu alisema hivyo.”

¹³⁷ Ibrahimu alitoa jasho kwa muda wa miaka ishirini na mitano kwa ajili ya mtoto huyo mchanga, bali aliwasili. Naam, bwana. Tofauti gani? Maadamu tu iwasili, hilo tu ndilo linalohitajika. Yeye aliliahidi, kwa hiyo dumu nalo.

¹³⁸ Na baada ya siku saba, ndipo asubuhi hiyo akaamka, na akasema, “Loo-loo, huyo hapo.” Loo, ni hisia ya jinsi gani!

Jamani, ungeweza kuwazia? Alijua ya kwamba ahadi ilikuwa karibu. Kwa nini? Angeweza kuhisi...Asubuhi hiyo kabla jambo lolote halijatukia, angeweza kusikia, huko mbali sana, mngurumo, dirisha hilo lililofunguliwa juu, labda futi ishirini upana au chochote kile, dirisha hilo kubwa huko juu.

¹³⁹ Mwajua, hiyo ardhi yenye joto iliyokauka na jua hilo kali, ambalo...Unajua unapopata kipindi kikavu sana kwa muda mrefu, halafu kwa mbali unaweza kuhisi upepo huo baridi ukiingia kutoka kwenye mvua hiyo? Alijua ilikuwa inakuja.

¹⁴⁰ Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu siku hizi. Mnajua, watu wanaangalia kote, wanasema, “Loo, bomu la atomiki! Tutajenga kimbilio la cheche za mnururisho. Tutafanya *hivi*.” Upuuzi. Upuuzi. Mnahofia nini hivi?

¹⁴¹ Nuhu akasema, “Mimi... Hilo linasikika tu kama vile Yeye alivyoniambia.” Hilo ni lile lile sasa, inasikika tu kama vile Yeye alivyoniambia. Naam, bwana, lilinibadilisha. Nami ninaamini ya kwamba Kuja kwa Bwana kumekaribia sana tunaweza tu kuhisi upepo unaotoka kwake. Hilo ndilo linalowaogopesha watu na kulifanya Kanisa kuwa tayari kuninii...kwa ajili ya Unyakuo, kunyakuliwa. Hakika, tuko katika wakati wa mwisho, hakika.

¹⁴² Kwa hiyo muda si muda mwajua, mvua ikaanza kunyesha na mafuriko yakaanza kupanda, barabara zikajaa maji, siku baada ya siku baada ya siku, na hatimaye, yakapanda futi ishirini juu ya mlima ulio mrefu kuliko yote, nao wakaangamia majini, wasioamini wote, lakini Nuhu akaelea moja kwa moja kupitia humo. Um-hum. Amina. Naam.

¹⁴³ Loo, liaminini Neno la Mungu, haidhuru jinsi lisivyo la kisayansi, liaminini, maana kama linaweza kuthibitishwa, basi haliwezi kuwa ni imani tena. Huna budi kuliadini wakati haliwezi kuthibitishwa, hu—huna budi kuliadini.

¹⁴⁴ Hukufanya upoteze imani katika Neno, uh, katika Neno la Mungu, bali wanataka kuchukua sehemu yao ya kiakili na kufanya hivyo. Vema. Wanasema, “*Hili ndilo*.”

¹⁴⁵ Sisi, Biblia ilisema, ya kwamba, hatushindani miereka, kwa nyama na damu, bali twashindana na nguvu za rohani. Sasa, kama tu mngotambua hilo, nilisema muda mfupi uliopita, tumefufuka pamoja Naye sasa. Hutakufa, tayari umekufa. Unaona? Lakini roho zetu ni hai ndani Yake. Kwa hiyo hatushindani na mambo ya kawaida, ya kisayansi, tunashindana na nguvu za rohani.

¹⁴⁶ Mwajua, wapiga miereka, wanafanya mazoezi ya kuvunja misimamo na kadhalika, bali huvunji misimamo, la. Ungeweza kuwazia mwanamiereka akitokea sasa, jamani, huku kucha zake zimepakwa rangi, viwiliwili vikiwa vimepambwa kila namna ya shanga za dhahabu? Anaonekana kama mwanamieleka mzuri sana, lakini kama hiyo ni ya kiakili tu, kama hana

nguvu zilizofichwa pale, kama hilo ni la kiakili tu, kama hana nguvu zilizofichwa mle, ambapo, wakati adui yake anapompiku, kwamba anaweza kumvuta amtoe hapo, haleluya, shanga zake za kiakili alizojifunga na kila kitu hazitaleta tofauti kubwa.

¹⁴⁷ Kwa hiyo akili zetu zote hazina maana kama hakuna nguvu zilizofichwa za Roho Mtakatifu mle, haleluya, kuvunja ngome ya ibilisi. Lakini sisi, tunapigana miereka, tunapigana miereka sio kwa saikolojia ya kiakili iliyovalia nadhifu, bali tunashindana kwa nguvu na ahadi ya Mungu ambayo inaweza kuvunja mshiko wowote juu ya ibilisi yeyote wakati wowote. Yesu, Bwana wetu, alithibitisha hilo alipokuwa Imanueli, Mungu Mwenyewe aliyefanyika mwili miongoni mwetu. Na wakati alipokutana na Shetani, kuonyesha ya kwamba Shetani angeweza kushindwa kwa Neno, kila wakati Shetani angemjia, Yeye alisema, “Imeandikwa. Imeandikwa.”

¹⁴⁸ Loo, jinsi ningetaka kuchukua wakati hapa kwenye muhtasari fulani nilioandika hapa, juu ya mambo ambayo Yeye alisema, ni mara ngapi Yeye alivunja nguvu za Shetani kwa “Imeandikwa!” Loo, jamani! Ikionyesha ya kwamba mtu huyo aliyeimarishwa nyuma ya Neno la Mungu anaweza kupaza sauti, “Imeandikwa, mwachilie. Achilia, Shetani, kwa maana imeandikwa,” kama unasimama nyuma ya Neno. “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu liko ndani yenu, ombeni mtakalo.” Hiyo ni kweli. Haliwezi kukosea, hilo halina budi kuwa sahihi.

¹⁴⁹ Naam, tunahitaji hizo nguvu zilizofichika kama alivyokuwa nazo Samsoni. Nimeona picha ya kiakili ya Samsoni iliyochorwa na mtu fulani, alikuwa na mabega, kweli, siamini mtu huyo angalitoshea kusimama jukwaani. Sijawahi kuona mabega kama hayo! Hilo lisingekuwa ni fumbo, jinsi ambavyo angeweza kumnyanyua simba, kumrarua vipande, ama kuyanyanyua malango na kupanda kilimani nayo, ama kitu kama hicho. Isingekuwa ni fumbo, mtu mkubwa hivyo, lakini alikuwa ni maskini mbilikimo mwenye nywele za kipilipili, karibu namna *hiyo*, mvulana mdogo wa mama, mawimbi madogo ya nywele yaliyoning’inia chini.

¹⁵⁰ Lakini mahali kitu hicho kilipokuwa, wasingeweza kuelewa mahali ambapo angeweza kuchukua mfupa wa taya la nyumbu na juu ya hizo helmeti zenye unene wa karibu inchi moja na nusu, na maskini mfupa huo wa taya ungalivunjwa kwa mshindo wa kwanza, maskini mfupa wa taya uliokauka, lakini aliwapiga tu hao Wafilisti kulia na kushoto nao. Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni nguvu zilizofichika. Jambo ndilo hilo. Hawakujua zilikuwa wapi. Mnaona?

¹⁵¹ Hivyo ndivyo Kanisa lilivyo siku hizi, Wana Nguvu zilizofichika, loo, jamani, Kitu fulani kinachowaimarisha. Ni kitu gani? Ni Neno, dhihirisho la neema ya Mungu pamoja na watu Wake. Um-hum. Naam, bwana. Naam, kama huna Nguvu

zilizofichika. . . Siku hizi tunasoma shuleni, tunawapeleka watoto wetu kwenye shule za Biblia, hilo ni sawa, kumbukeni, hakuna kitu dhidi yake, hata kidogo, lakini hilo silo lililo muhimu.

¹⁵² Mwajua, Petro usiku huo, loo, jinsi alivyokuwa. . . wakati kuhani mkuu alipokuja, mtumishi wake, aliuchomoa upanga wake, angeweza kupigana, aliuchomoa upanga wake na kukata sikio lake. Naam, alikuwa na—na nguvu nyingi mikononi mwake, bali alipofikia kwenye ujasiri wa kiroho, hakuwa nao, alilikana Neno la Bwana, kwa sababu Kristo alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, kwa hiyo akalikana.

¹⁵³ Loo, jinsi ningetaka kukaa kwenye hilo kwa dakika chache, jinsi ambavyo Neno hilo. . . Alisema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizitenda hizo kazi za Baba Yangu, basi aminini hizo kazi.” Yeye alisema, “Enyi wanafiki, mnaweza kuona ishara angani,” kuhusu, mwajua, kuja kwa mvua na kadhalika, lakini kasema, “ishara za wakati hamwezi kuzitambua. Kwenu, kama mngalinijua Mimi, mngaliijua siku Yangu.” Mnalipata?

¹⁵⁴ Naye Petro aliona hayo yote, na kusikia hayo yote. Na kwa mkono ambao ungeweza kukata ninii la mtumishi huyo wa kuhani. . . Hapana shaka alikuwa stadi wa kutumia upanga kweli, kwa sababu alikuwa mtumishi wa kuhani, naye alikuwa mlinzi, alikuja huko nje, angeweza kutumia mkuki wake, bali Shetani alikuwa ninii sana, ama—ama, Petro alikuwa bora zaidi kwa mkuki, ama, kwa upanga wake kuliko huyu alivyokuwa kwa mkuki wake, akayakatilia mbali masikio yake.

¹⁵⁵ Lakini ilipofikia kwenye ujasiri halisi wa ndani kabisa, yeye hakuwa nao. La, hakuwa nao. Wakati alipokuwa ameliona hilo Neno. . . Sasa, nitajisikia kubarikiwa. Alipokuwa ameliona Neno hilo likidhihirishwa, na kujua ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo siku ya Hilo kuwa pale, na kuliona likithibitisha vile hasa Mungu aliyosema lingefanya, na halafu kwa nguvu zake zote za kiakili, utu wake wote wa kimwili. . .

¹⁵⁶ Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Watu wanaokuja tu na kuandika majina yao kwenye kitabu, wale wanaopeana mikono na mhudumu, ndipo inapofikia kusimama ofisini naye bosi anapitisha kinywaji, watakinywa, wanahofia kazi yao. Inapofikia kulipia zaka zako kanisani mwako, unaogopa kufanya hivyo, kwa sababu unahofu utakufa njaa, huku unajua Mungu alitoa ahadi ya kwamba atakushughulikia, mambo haya yote.

¹⁵⁷ Kisha unapokuja kanisani, naye Roho Mtakatifu anashuka miongoni mwa watu, na Kitu fulani moyoni mwako kinakwambia, “Hili ndilo, hilo ndilo Neno.” Unapoona ubatizo na kila kitu kingine kikitolewa katika Neno, unaogopa

kuuchukua. Kuna shida gani? Huna ujasiri, ujasiri wa kiroho kusimama.

¹⁵⁸ Kwa hiyo hakuwa nao. Angeweza kupigana, angeweza kusema, “Mimi ni wa *Hiki-na-hiki*, nataka mfahamu.” Lakini hivyo sivyo ilivyokuwa. Lakini alipoona Neno likidhihirishwa kisha akalikana, loo, hilo lilikuwa ni jambo la kuchukiza jinsi gani!

¹⁵⁹ Lakini, ndugu, baada ya Pentekoste alipanda akaenda na kuvaa silaha zote za Mungu, hakika alikuwa na ujasiri wakati huo. Mwangalie jamaa yule yule, mwaminio wa Kristo, aliyemfuata saa baada ya saa, bali alikuwa tu ameona Neno kwa andiko, alikuwa ameliona tu likidhihirishwa, lakini sasa lilikuwa *ndani* yake. Utukufu! Haleluya! Neno la... Neno motomoto la Mungu lilikuwa likiwaka katika mwili wake mwenyewe. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu ndani yako. Amina. Mungu, Kristo, tumaini la Utukufu lililodhihirishwa katika mwanadamu Kanisani. Mungu alijua alichokuwa akifanya. Naam, bwana. Haikuwa ni kutumaini *hili*, ama *lile*, ama *linginelo* tena, ilikuwa ni Mungu Mwenyewe. Amina.

¹⁶⁰ Ndipo akasimama pale na kusema, “Enyi watu wa Israeli, nanyi mkaao Uyahudi, sikilizeni sauti yangu, hawa hawajalewa kama mnavyodhanja. Hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, ‘Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitaimwaga Roho Yangu.’ Whiu! Whiu! “juu ya wote wenye mwili, na wana wenu na binti zenu watatabiri. Juu ya wajakazi Wangu wanaume na wanawake nita-...” Amina. Hakuna mambo ya kiakili juu ya jambo hilo, alikuwa na kitu fulani.

¹⁶¹ Ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa amevaa silaha zote za Mungu. Whiu! Hana hata angalau mavazi ya kuhani mkuu, bali alikuwa na kitu fulani ndani yake, silaha za Mungu huingia ndani, nguvu za kiroho, zilizofichika za Mungu ambazo jicho la kiakili halizioni hata kidogo. Yesu kamwe hakusema, “Uliliona?” Alisema, “Uliliamini?” Amina. Naam, bwana. Loo, jamani!

¹⁶² Mara nyingi nimefanya *kosa* dogo fidhuli. Huenda ikawa, sikukusudia kufanya hivyo, lakini labda nililiseba vibaya, lakini sikuzote nilisema, “Petro alisema basi, ‘*Hili ni lile*,’ na kama *Hili* si *Lile*, nataka kuliweka *Hili* hata *Lile* litakapokuja.” Ni—ni—ni—ninaamini *Hili* ndilo *Lile* hata hivyo, maana ilihitaji maskini mwenye dhambi kama mimi na kunifanyia jambo fulani, liliweka upendo moyoni mwangu ambao unawaka moto. Loo, jamani! Na sasa, umekuwa ukiwaka moto kwa muda wa miaka thelathini na ungali unawaka, ukiangaza zaidi wakati wote ninapoelekea Mahali hapo. Naam, bwana. Loo, jamani, Neno Lake!

¹⁶³ Petro akisimama pale akamkana, lakini siku chache tu baadaye alisimama mbele ya umati wote. Kwa nini? Ndipo alikuwa na upande wa kiakili, ule upanga, “Tulikuwa na milioni

moja zaidi mwaka uliopita. Tulikuwa na *kadhaa* katika dhehebu letu.” Lakini sasa ana kitu fulani ndani. Loo, jamani! Amevaa silaha zote. Loo, jamani! Ni ajabu jinsi gani! Loo, naam. Vema.

¹⁶⁴ Loo, Mungu hujiwasilisha Mwenyewe katika jeshi Lake basi. Mnaamini hilo? Sasa, Mungu alisema, “Niliwatumia Neno, Hawa alilikanyagia tu chini moja kwa moja, hakuliamini, nikalidhihirisha, nao wakalisulubisha, ninachoka tu, naja Mwenyewe.” Kwa hiyo huyu hapa anakuja, Mungu ndani yako. Mungu juu yetu, Nguzo ya Moto; Mungu pamoja nasi katika Yesu Kristo; Mungu ndani yetu, Roho Mtakatifu. Ni kitu gani? Neno lile lile, Mungu yule yule. Amina.

¹⁶⁵ Hakuna tena kutumainia kitu kingine chochote, Mungu amekuja Mwenyewe. Hii ni kazi ya Mtu mzima, kwa hiyo Yeye alishusha tu yote, kisha akashuka Mwenyewe, “Haitawabidi kufanya lolote kulihusu, acheni tu wajisalimishe Kwangu nami nitatembea ndani yao, nitaongea ndani yao, ninene ndani yao, nifanye kazi ndani yao, kikamilifu.” Loo, jamani! Jambo ndilo hilo. “Nitafanya ninii, kufanya. . . Nitafanya hizo kazi, acheni tu wajinyenyekeze, acheni wajifanye tupu, nitamshinda adui Yangu huko nje kupitia kwao.” Jambo ndilo hilo. Huwezi kufanya hivyo mwenyewe sasa, huwezi kumstahimili, bali kama utamruhusu tu Mungu afanye hivyo, aingize Neno ndani yako, basi itakuwa, yote yatashugulikiwa.

¹⁶⁶ Sasa, Mungu aliliimarisha jeshi Lake. Kwa kitu gani? Mwenyewe, katika mfano wa manabii, mitume, waalimu, wachungaji. Yeye alifanya nini? Mungu alikuwa akifanya nini? Sikilizeni, hivi mliwahi kuwazia hizo ofisi za Kanisa ni nini? Ni vazi la Mungu, vazi la ndani, mtume, nabii, mwonaji. Kuliona kabla Shetani hajalifikia, tayari amelisema. Ni kitu gani? Mungu amevaliwa Kanisani Mwake, ofisi hizi ni vazi la Mungu. Unapoona ofisi hizo, wachungaji, waalimu, wainjilisti, hizo ni nini? Hizo ni vazi la Mungu, Uwepo wa Mungu, Roho wa Mungu, na kama. . . akitenda kazi kupitia kwa mwanadamu.

¹⁶⁷ Na kama ofisi hiyo ikikanusha lolote la Neno hili, basi hayo si mavazi ya Mungu, mnaona. Mnaona? La, siyo, huyo ni mbwa mwitu aliyevaa ngozi ya kondoo. Mwangalie jamaa huyo, jihadhari naye. Lakini anapochukua tu yale Neno lisemayo, kumbukeni, huyo ni Mungu, maana yeye ananena Neno Lake. Mnaona? Lakini kama akisema, “Vema, si. . .” Loo, loo, loo, loo, loo, loo, jamani! Ondokeni, enyi kondoo, ondokeni!

¹⁶⁸ Kwa nini akafanya hivyo? Sasa, ulimwengu usingeamini ya kwamba Mtu huyo alifufuka tena, hawakuliamini kwanza kabisa, walisema, “Vema, vema, wao—wao—walimwiba, wanafunzi Wake walikuja, wakamwiba. Naam, ninii. . .” Hawakuamini jambo hilo, walilionna hilo.

¹⁶⁹ Ndipo Mungu akasema, “Sasa, ngojeni kidogo, nitakuja na kuwa ndani Yake mimi Mwenyewe. Nitakabiliana na adui

Yangu Kanisani Mwangu, nitamshinda kwenye misingi yake mwenyewe.”

¹⁷⁰ Alifanya hivyo wakati mmoja. Naam. Mnajua yale aliyofanya? Alimchukua Musa na kumketisha papo hapo nchani mwa pua yake, na kumwacha adui amlishe na kumlea, moja kwa moja namna hiyo, akashuka, na kumshinda adui na kumzamisha chini ya Bahari ya Chumvi. Uh-huh. Hiyo ni kweli. Hakika, alifanya hivyo. Kisha kuwazia. . .

Ee Mungu Asiye na kikomo! Tuna nini cha kuhofia? Yeye ni Mungu. E—endelea tu na umwamini Yeye. Hakika.

¹⁷¹ Sasa, Yeye alisema angefanya, angefanya nini? Angekuja na kujithibitisha Mwenyewe katika Kanisa Lake, Nao wangethibitisha kufufuka Kwake kwa kazi Zake. Mnaona? Naam, Yohana 14:12, nafikiri hiyo ni kweli, naam, Yohana 14:12, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.”

¹⁷² Mnaona, ni kitu gani? Sasa, unasema, “Ninaamini,” hilo ni neno tu, bali kama kweli unaamini, hilo ndilo *Hili*. Kama Yeye ni Neno, basi huna budi kuliadini Neno lote, “Yeye aniaminiye Mimi wote,” (usiamini tu sehemu Yake, “niamini Mimi wote,”) “basi kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya,” kwa kuwa Yeye angali ni Neno lile lile. Kwa hiyo kama ni Neno lile lile, lingefanya kazi zile zile.

¹⁷³ Kama huyu Roho Mtakatifu aliye hapa leo, kama si Neno lile lile ambalo lilikuwa hapo mwanzo. . . kama Ndilo, litafanya kazi zile zile. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Loo, ningetaka kudumu juu ya hilo kwa muda kidogo, lakini inachelewa sana. Kwa nini? Neno lile lile, kazi zile zile, unaona, maana Yesu alikuwa ni kazi za Mungu, tunajua hilo.

¹⁷⁴ Mathayo 28 ilisema, “Nitakuwa pamoja na jeshi Langu, isitoshe, bali ninaenda *ndani* ya jeshi Langu.” Loo, jamani! Loo, jamani! Wazieni jambo hilo. Shujaa wetu mkuu, Ushindi mkuu, Jemadari-Neno, ndani yetu. Neno, aliyefanyika mwili na akashinda kila pepo, kila maradhi, hata mauti, kuzimu, na kaburi, Jemadari yuyo huyo yuko ndani yetu, pamoja nasi. Muda gani? “Hata ukamilifu wa dahari,” moja kwa moja na kuendelea. Wazia jambo hilo, Yule anayeongoza vita.

¹⁷⁵ Kila nguvu za adui zimeshindwa. Wakati alipokuwa hapa duniani, alilichukua Neno na kushinda kila kitu alichokuwa nacho Shetani, alishinda mauti, alishinda kuzimu, akashinda kaburi, akafufuka katika siku ya tatu, kisha akarudi na sasa anaishi katika Kanisa Lake, huyu Neno-Shujaa mkuu, yule Shujaa aliyekuwa Neno.

¹⁷⁶ Naye Shujaa yuyo huyo ambaye ni Neno yuko ndani yetu, akiishi Mwenyewe, akiitikia kila alama ya kufufuka Kwake na Kuja Kwake. Amina. Anafanya hivyo leo, katika wakati huu wa

jioni, wakati Nuru kuu za jioni zinapoanza kuangaza. Haleluya! Huyu Shujaa mkuu, Kristo, tayari ameshinda, hakuna lolote kwangu kufanya, ni kufuata tu. Amina. Amina. Kila nguvu zimeshindwa. Nakwepa Maandiko mengi hapa. Ninapenda hilo.

¹⁷⁷ Ninawazia jambo hilo, wakati mmoja hapa miaka michache iliyopita, huko chini Jeffersonville, Kampuni ya Mafuta ya Pfau ilishika moto. Nasi tuna lundo la vyombo vidogo vya zimamoto kule chini, nao walipokuja huku walionekana kama mtoto mwenye bomba huko nje uani. Kiongozi wa zimamoto alikuwa akikimbia-kimbia pale, mwajua, akisema, “Um, uh, nyunyizia kidogo juu. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . *hapa*,” akitafana hiyo biri, kama maksai wa Teksasi aliyeng’olewa pembe, akisema, “*Hapa*, nyunyizia kidogo *hapa*.” Ndipo zimamoto wote wakakimbia huku na huku wakivuta bomba, “Naam, Bwana, Mheshimiwa, Bwana.” *Shuush, shuush, shuush, shuush, shuush, shuush!* Moto ukiendelea kuwaka moja kwa moja, ukiwaka moja kwa moja.

¹⁷⁸ Baada ya kitambo kidogo wakapiga simu Louisville, kuvuka daraja lile likaja gari kubwa la zimamoto. Mara waliposimama, walikuwa na ngazi ya kukunja, ni nani aliyekuwa amesimama. . . ? Kabla ngazi haijaanza, yule kiongozi alitangulia mbele; wakati ngazi ilipopanda, kiongozi wao alikuwa juu. Alipofika dirishani, hakusimama hapa, ati “Rusheni maji kidogo *hapa*, rusheni maji kidogo *pale*.” Alifanya nini? Alichukua shoka na kulitupa kupitia dirishani na kusema, “Njoni, wavulana!” Utukufu! Hivyo ndivyo Kiongozi wetu alivyofanya. Haleluya! Aliongoza njia hata mautini, kuzimu, na kaburini, na kusema, “Njoni, enyi wavulana!” . . . ? . . . namna fulani ya kanuni za imani. Loo, “Njoni!” Yeye huongoza njia. Haleluya! Dakika chache moto ukazima.

¹⁷⁹ Hebu na avunje madirisha na kuta za kanuni zenu za kale na aingie wakati mmoja. Ushirikina wote na pepo wataondoka. Utukufu! Mambo yatabadilika. Hatuhitaji majitu wakubwa wa kielimu, tunamfuata tu yule Kiongozi. Kiongozi alishuka moja kwa moja, na kulichukua Neno la Mungu na kulivunja akaingia moja kwa moja, kasema, “Haya basi.”

¹⁸⁰ Mwajua, ninaambiwa ya kwamba jeti, baada ya kwenda kasi sana, inafikia kizuizi cha sauti, halafu inabidi tu itetemeke na kutikisika mpaka ipite kizuizi hicho cha sauti, na baada ya kupita hicho, inakuwa huru tu. Loo, hivyo ndivyo ilivyo, ndugu, unaweza tu kufia kila kitu, mpaka ufikie kizuizi cha dhambi, huko ni kutokuamini, upite hayo, na kila kitu kitaenda sawa. Unapoliamini Neno la Mungu unaweza kumtikisa kila ibilisi atoke kwako na kukimbia, kila kitu. Amina. Vaeni silaha zote. Naam, bwana.

¹⁸¹ Kiongozi anatuongoza, akituongoza Nyumbani. Amina. “Njoni Nyumbani. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao

mengi, kama sivyo, ningaliwaambia. Sitawaacha ninyi yatima. Nitakuja tena na kuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona. Kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Kiongozi, akiongoza. Amina.

¹⁸² Bwana wangu anajua njia ya kupitia nyikani, yote ninayopaswa kufanya ni kufuata. Amina. Sikia *pum, pum, kukanyaga* kwa jeshi, likienda kwa ushindi, bila kujali kutokuamini huku kwote huku maskini kunguru na mwewe wakipiga kelele hapa, sisi ni tai, hebu turuke juu kutoka kwa kila kitu, ndugu. Amina.

¹⁸³ Hapa wakati fulani uliopita jeshini, wakati taifa letu lilipotoa helmeti kwa mara ya kwanza, loo, jamani, maskini kuruta yule hakutaka kuvaa hiyo, ilionekana si ya lazima, bali alipoingia vitani aliihitaji. Mungu hatoi chochote, isipokuwa ana haja nacho. Kila kitu anachokupa, afadhali ukichukue, maana utakihitaji.

¹⁸⁴ Maskini kuruta mwenye mkoba wa ratili tisini mgongoni mwake mazoezini, amevaa suti yake mpya, mwajua, wala haoni chochote cha lazima, kubeba mkoba huo wa ratili tisini pamoja na sururu hizi zote, na sepetu, na makombora ya mkono, na kadhali, lakini acha aingie vitani mara moja! Wakati utakuja ambapo lazima uwe nao. Hiyo ni kweli.

¹⁸⁵ Hiyo ndiyo sababu Mungu mwenye hekima yote aliliandaa jeshi Lake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Alijua hawa majitu wa kiakili wangesimama katika siku hizi za mwisho. Haleluya! Alijua wangesimama, nao wangeweza kueleza, kwa hekima yao kuu, nguvu za Shetani. Petro alisema, “Wao ni kama simba angurumaye, akimeza atakacho.” Naam.

¹⁸⁶ Lakini Yeye alisema, “Sitawaacha yatima, naja tena, nitakuwa pamoja nanyi.” Aliliandaa jeshi Lake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kasema, “Pandeni kule, kila mmoja wenu mkangojee.” Luka 24:49. “Tazama, nawaleta juu yenu ahadi ya Baba Yangu, lakini ngojeni katika mji wa Yerusalemu, mpaka, mpaka mtakapovikwa Uwezo utokao Juu. Akiisha huyu, Roho Mtakatifu kuwajilia juu yenu, basi mtakuwa mashahidi wangu, Yerusalemu, na Uyahudi,” Matendo 1:8, “hata pande za mwisho za ulimwengu.”

¹⁸⁷ Wakati Roho Mtakatifu aliposhuka na Moto ukaanza kuwashukia, wote walijazwa na Roho Mtakatifu, wote wakakimbia pamoja huko nje mitaani, kasema, “Haya yote yanamaanisha nini hapa? Mbona twasikia kila mtu kwa lugha yetu wenyewe, tuliyojaliwa nayo?” Wakaendelea na kutaja lugha mbalimbali walizokuwa wakizungumza. Ndipo wengine wakadhihaki wakisema, “Hawa wamejaa divai mpya.”

188 Lakini Petro akasimama katikati yao akasema, “Enyi watu wa Yerusalemu, nanyi mkaao Uyahudi, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu: Hawa hawajalewa, kama mnavyodhania, mbona, ni—mbona, ni saa tatu tu mchana.” Saa tatu asubuhi, vilabu hata havijafunguliwa bado. Mnaona? Hili ndilo, naam, bwana. “Hili silo lile, bali hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli,” akirudi kwenye Neno hilo. Naye akalikata, na kulikata upande mmoja hadi mwingine. Amina.

Na hao wazee wakachomwa moyoni mwao na kusema, “Waume na ndugu zetu, tufanye nini?”

189 Yeye akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wote walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Naam, bwana. Hicho hapo kielelezo, hivyo ndivyo alivyosema ifanywe, lifuatilie mara moja uone kama ni kweli. Amina. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Ninapenda hilo, maana ni ahadi.

190 Katika Agano la Kale wakati mana ilipoanguka, ile mana ya kwanza iliyoanguka, Mungu aliwaambia watoke waende kule na kuchukua pishi nzima yake, pishi nzima, na kuweka katika Patakatifu pa patakatifu; kama walijaribu kuihifadhi, iliingia mchwa wadogo, vifurukuta mkia ndani yake. Mnajua maskini vifurukuta mkia ni nini, tunavyowaita huko chini kusini. Wanaingia kwenye birika na kila kitu, mwajua, na wa—wadudu wadogo. Hiyo ndiyo shida ya ujuzi wa watu wengi sana, una wadudu fulani ndani yake, mnaona, ukijaribu kuuhifadhi juu ya ule uliokuwa nao miaka miwili iliyopita. Jamani, hebu tuupate sasa hivi tena. Mnaona?

191 Mana hiyo ilishuka kila usiku, nayo Mana hiyo ilikuwa ni Kristo. Mnaona, huwezi kudumisha tukio la jana, huna budi kuwa na moja sasa hivi. Unaona? Hiyo ni kweli, leo. Lakini kulikuwa na baadhi yake iliyowekwa katika Patakatifu pa patakatifu, ambayo ilidumu, Alisema, “Vizazi vyote vitakavyokufuata, watakapofanywa kuhani katika ukuhani, wanaweza kuuma mana ya asili iliyoanguka mwanzoni.” Mnaona?

192 Angalieni, sasa Petro alisema jambo lile lile. Yeye... Walisema... Yeye alisema, “Hili ndilo lile, hili ndilo.” Akasema, “Sasa, tubuni ninyi nyote, mkabatizwe katika Jina lake Bwana Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu,” sasa sisi ni makuhani wa kifalme, “na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

193 Kila mmoja, atapitia kwenye fomula hii, aje na kutubu kwelikweli, na kubatizwa, mtazamieni Mungu, Yeye atawapa si

funda moja, bali ya kujaza moyo, si kitu fulani, si mhemuko fulani ama saikolojia fulani, bali Roho Mtakatifu halisi, yule wa asili aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste, upate Kitu kile kile, naam, kama ukifuata maagizo.

¹⁹⁴ Ni kama tu kutoa dawa, madaktari wengi sana siku hizi. . . Vipi kama ulimchukua m—mwuza dawa wala hukujaza maagizo jinsi daktari alivyoyaandika? Unajua nini kingetukia? Kukuua. Hiyo ndiyo shida, mna wafuasi wengi sana wa kanisa waliokufa. Utukufu! Ndugu, usiyachezee, hivyo ndivyo daktari alivyoandika. Yachukue tu jinsi yalivyo, hilo tu ndilo likupasalo kufanya. Mna wauza dawa matapeli wengi kupita kiasi. Naam, bwana.

¹⁹⁵ Alijua kile jeshi Lake lilichohitaji, hiyo ndiyo sababu aliwaandaa kwa Roho Mtakatifu. Walijua ingewabidi kuninii. . . Ingembidi kuwa nao, ingewabidi kuwa na Yeye. Naam, bwana. Alijua kuwa shahidi hodari, wao, kushuhudia kufufuka Kwake, ingewabidi kuwa na Roho Mtakatifu.

¹⁹⁶ Sasa, Yeye alisema, Marko 16, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili.” Kwa maneno mengine, mkazidhihirishe hizo nguvu. “Na ishara hizi zitafuatana na hao wanaoikubali Injili.” Mnaona?

Sasa, kusema tu maneno ya kiakili. La, la. Wasingeweza kufanya hivyo kwa maneno ya kiakili, Neno hilo halina budi kufanyika mwili, kudhihirishwa. Mnaona?

¹⁹⁷ “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, watahika nyoka, watakunywa vitu vya kufisha, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Kudhihirisha nguvu za Roho Mtakatifu, Neno lililodhihirishwa. “Mambo haya ninayowaambia yatatimia,” kama Neno la kuhuisha, “yatatimia.” Una nguvu za Roho Mtakatifu ndani yako. Si wewe, ni Roho Mtakatifu anayefanya jambo hilo. Unaona?

¹⁹⁸ Sasa, ili uwe shahidi mzuri wa Mungu inakubidi kuwa na Roho Mtakatifu, kwa sababu bila Roho Mtakatifu huwezi kulifanya hilo liishi. Nawe unajua utakalofanya? Utachukua wazo la jitu fulani la kielimu kulihusu, na kulikwepa, na kusema, “Hilo lilikuwa tu kwa ajili ya mitume.” Loo!

Kuna watu karibu kila mahali,
Ambao mioyo yao inawaka moto
Kwa ule Moto ulioshuka kwenye Pentekoste,
Uliowasafisha na kuwafanya safi;
Loo, unawaka moyoni mwangu sasa,
Loo, utukufu kwa Jina Lake!
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Hivi hamfurahii jambo hilo?

Ingawa watu hawa huenda wasijifunze kuwa,
 Au kujivunia sifa za ulimwengu,
 Wote wameipokea Pentekoste yao,
 Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
 Nao wanatangaza sasa, kwa umbali na upana,
 Nguvu Zake zingali ni zile zile,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

¹⁹⁹ Loo, ninafurahia jambo hilo. Naam, bwana. Naam, bwana. Ingekubidi kuwa na Roho Mtakatifu kudhihirisha nuru hizi za jioni, hiyo ni kweli, kufanya Mar- . . . Waebrania 13:8, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele,” halisi. Hiyo ni kweli.

²⁰⁰ Vaeni silaha zote za Mungu. Usizitumie kama nguo, au kujionyesha tu huku na huko. Lakini ni kitu gani? Vaeni silaha zote za Mungu, na ili kwamba, unapovaa silaha za Mungu, unaweza kuchukua upanga wa Mungu, kwa imani, na kufanyiza njia yako kupitia ahadi yoyote ambayo Mungu alikuahidi.

²⁰¹ Kama ugonjwa ukikuzuia, ukatilie mbali na kuuondoa njiani, ni ahadi ya Mungu. Kama dhambi ikikuzuia, ikatilie mbali na kuiondoa njiani. Hiyo ni kweli. Silaha zote! Ibilisi akikurushia mshale, uondolee mbali na uendelee kukata. Hiyo ni kweli.

Hima askari Wakristo!
 Wakienda kama vitani,
 Pamoja na msalaba wa Yesu
 Ukitangulia mbele; (Haleluya!)

Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao; (Haleluya!)

Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Hivi hamfurahii jambo hilo? Hakika mna furaha. Naam, bwana.

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha
 juu,
 Wote wakiomba katika Jina Lake,
 Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
 Ndipo nguvu za utumishi zikaja;
 Sasa, yale aliyowafanyia siku hiyo
 Atakufanyia vivyo hivyo,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.
 Mmoja wao, mmoja wao,

Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao;
 Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

²⁰² Huko Memphis siku moja, mmenisikia nikisimulia, nadhani, nililiwazia tu, nilikuwa nikija, nikiimba ule wimbo mdogo. Ndege ilikuwa imesimama, dhoruba ilitokea, usiku uliotangulia, nami nilikuwa nikitoka hu—huko Dallas, Teksas, nayo ilisimama huko Memphis, dhoruba ikaishusha.

²⁰³ Wakaniweka kwenye hoteli kubwa, wakaniambia kesho yake asubuhi wangenipigia simu, saa moja. Nilikuwa ninaenda kutuma barua mapema sana, yapata saa kumi na moja, sikulala sana, basi njiani nikishuka Roho Mtakatifu akasema, “Geuka, urudi upande ule mwingine.”

²⁰⁴ Nikatembea mbele kidogo, na kulikuwako na vigurudumu na bunduki na kadhalika dukani, maskini polisi mkubwa wa Kiairishi amesimama pale, nikaenda kwenye vigurudumu hivi, na kuangalia juu chini, nikawazia, “Amecha kuniangalia.” Nikasema, “Bwana, huyo alikuwa ni Wewe?” Hivi hamwamini wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Bwana?

²⁰⁵ Kasema, “Geuka, na urudi upande ule mwingine.” Nikaanza tu na kurudi. Nami nikavuka, nikaenda huko chini kusini mwa Memphis kule, nikafika miongoni wanakoishi watu weusi. Nami nilikuwa nikienda kule, nikawaza, “Jamani,” nikaangalia saa yangu, “wakati wa ndege kuondoka umewadia!”

Kitu fulani kiliendelea tu kusema, “Endelea mbele, mbele.” Jua lilikuwa kubwa limechomoza, mwajua.

²⁰⁶ Nilikuwa nikienda kule, na moja kwa moja nikaangalia, amesimama nje kwenye lango dogo, na hapo alisimama dada mweusi wa kawaida, alionekana kama mmoja wa hawa Shangazi Jemima, mashavu yake makubwa manene yakiwa yamening’inia pale. Machozi yalikuwa yakitiririka mashavuni mwake, akasema, “Habari za asubuhi, Kasisi.”

²⁰⁷ Nikasema, “Njema.” Nikasema, “Shangazi, ulijuaje nilikuwa kasisi?” Sasa, huko chini kusini hivyo ndivyo mhudumu anavyoitwa. Nikasema, “Ulijuaje nilikuwa kasisi?”

²⁰⁸ Akasema, “Aa, nilijua ulikuwa.” Kasema, “Kuna kitu kimoja ambalo nimekikosa tu,” kasema, “wewe,” kasema, “ulipaswa kuvaa suti ndogo ya kijivu, na kofia ndogo iliyowekwa kando ya kichwa chako,” kasema, “lakini uko wapi ule mkoba uliokuwa nao?” Nilikuwa tu nimeuweka chini.

Nikasema, “Niliuacha hotelini.”

Akasema, “Nilijua utakuja.”

Nikasema, “Jina langu ni Branham. Hivi ulijua . . . ?”

Kasema, “La, Bwana.” Kasema, “Kasisi Branham, sikujui mimi.” Akasema, “Lakini je, umewahi kusikia katika Biblia kuhusu yule mwanamke Mshunami?”

Nikasema, “Naam.”

²⁰⁹ Kasema, “Unajua, a—alikuwa na mtoto mchanga, alikuwa mkongwe sana asingeweza kupata mtoto, na hata hivyo akampata mtoto.” Kisha kasema, “Huyo Eliya, yule nabii, alienda na kumwambia kuhusu mtoto huyo mchanga maana alikuwa mwema kwa nabii huyu.”

Nikasema, “Naam, ninajua hadithi hiyo vizuri sana, Shangazi.”

²¹⁰ Akasema, “Vema, mimi ni mwanamke wa namna hiyo.” Naye akasema, “Nilimwomba Bwana, mimi na mume wangu, atupe mtoto. Nilisema nitamlea jinsi alivyomlea.” Kisha kasema, “Alitupa mvulana mzuri.” Kisha kasema, “Lakini mvulana wangu alichukua njia mbaya.” Kasema, “Alitoka akaenda miongoni mwa wenye dhambi na kadhalika, akapitia njia ya dhambi.”

²¹¹ Kisha kasema, “Yeye amelala mle ndani akifa, alipata ugonjwa wa zinaa.” Kisha kasema, “Yuko huko ndani akifa.” Kisha kasema, “Hatukujua hilo, sisi Wakristo hapa,” kasema, “ilichukua muda mrefu sana hata ikageuka kuwa kaswende.” Kisha kasema, “Yu—yuafa.”

²¹² Kisha kasema, “Daktari alikuja na kusema kwamba wasingeweza kumfanyia lolote. Damu yake ilikuwa zaidi ya nne nao wangempa Salvarsan 606, na zebaki, na kila kitu, bali haikufaa kitu. Nayo ilikuwa—ilikuwa imeenea sana, ilikuwa tayari imetoboa mashimo moyoni mwake.” Tena kasema, “Yuafa.” Naye akasema, “Kamwe nisingeweza, Kasisi, kustahimili kumwona mtoto wangu akifa.”

²¹³ Kasema, “Baba yake alienda kazini asubuhi ya leo.” Kisha kasema, “Usiku kucha nilikuwa macho, nami nikaomba, nikasema, ‘Bwana Mungu,’ kasema, ‘Wewe ni Mungu yeye yule aliyekuwa huko nyuma katika siku za Eliya.’ Kisha kasema, ‘Sasa, mimi—mimi—mimi ni aina ya mwanamke kama alivyokuwa, na Wewe umenipa mtoto wangu mchanga hapa,’ tena kasema, ‘amepitia njia mbaya, Bwana, bali nimefua kwenye mbao na kujaribu kukutumikia Wewe, na kwenda kanisani Mwako, na kuwasikiliza wachungaji Wako.’ Kisha akasema, ‘Ni—nilijaribu na kufanya kila kitu nilichoambiwa nifanye.’” Akasema, “‘Sitaki kumwona mtoto wangu akifa namna hiyo.’” Akasema, “‘Kama . . .’ Nami nikasema, ‘Bwana, nifanye nini?’”

²¹⁴ Kisha kasema, “Nilishikwa na usingizi, nami nikaota nilikuona ukishuka kuja barabarani. Nilipoamka Yeye akasema, ‘Nenda huko nje ukasimame karibu na lango.’” Na mgongo wake ulikuwa ungali umelowa maji. Alikuwa a—amejifunga shati la mwanamume kichwani mwake.

Nami nikaangalia kule chini, nikamwangalia, nikawazia. “Jamani!”

Akasema, “Hivi hutaingia?”

²¹⁵ Loo, jamani! Nikafungua lango lile la kale la nyuma, maskini kipande cha plau kimevekwa pale kwa ajili ya uzito wa lango, mnajua hizo ni nini. Nami nikaingia ndani. Nimekuwa katika majumba ya wafalme, mwajua, lakini kamwe sikukaribishwa zaidi ya nilivyokaribishwa katika nyumba hiyo ndogo ya watu weusi asubuhi ile, maskini sakafu, la, na maskini kitanda hicho cha chuma kilisimama pale, maskini. Bali hapo kitandani alikuwa amelala mvulana mkubwa mno, mwenye sura nzuri, alionekana kuwa na yapata ratili mia moja na tisini, mwenye nguvu tu, na mzito. Naye alikuwa na shuka mkononi mwake, ama kitu hicho kidogo juu yake, akisema, “Uhhh, uhhh, uhhh.”

Nikasema, “Habari za asubuhi, Bwana.”

²¹⁶ “Loo,” akasema, “Kasisi, hajajua chochote kwa siku tatu ama nne.” Kasema, “A—anafikiri ya kwamba. . . anafikiri yuko huko nje baharini ama mahali fulani pakubwa.” Kasema, “Yeye, alinena kuhusu giza, naye yuko kwenye mashua, wala hawezi kupata njia ya kurudi. Naye anasema. . . Hilo ndilo linalonivunja moyo.” Kasema, “Mimi, laiti ningalimsikia tu akisema amekoka.”

Nikasema, “Shangazi, mimi huwaombea wagonjwa.”

²¹⁷ Hakuvutiwa na jambo hilo, alitaka kumwona mvulana huyo ameokolewa, hilo ndilo alilotaka kuona, mvulana huyo akiokolewa, alijua angemwona tena Upande ule mwingine basi. Akasema, “Sasa, amechukua njia mbaya. Hivi hutamwombea?”

Nikasema, “Vema, na tuombe.” Nikasema, “Vema, na tuombe.”

²¹⁸ Kwa hiyo tukapiga magoti, nikasema, “Shangazi, wewe omba kwanza.” Loo, jamani! Wakati yule mtakatifu mzee mpendwa alipoanza kuomba, wewe. . . halikuwa jambo jipya kwake. Alizungumza Naye kana kwamba alikuwa amezungumza Naye hapo awali. Mnaona? Naam, alifanya hivyo. Nilihisi tu mzizimo ukiingia mwilini mwangu namna *hiyo*. Nikawaza, “Ee Mungu, ulipataje kuniongoza huku chini namna hii?” Nikawaza, “Ee Mungu, Wewe ni wa ajabu sana!”

²¹⁹ Nilimwangalia, nami nikasimama, na kumwangalia, naye, machozi yakitiririka. Akasema, “Bwana, mimi hapa.” Akasema, “Ni—ni—niliomba, nawe ukanipa ndoto na kusema kasisi huyu alikuwa anakuja, nami nikangojea papo hapo.” Ninaamini Mungu hufanya kazi kwenye miisho yote miwili ya mstari, hiyo ndiyo sababu nisingeweza kwenda kwenye ndege. Kasema, “Nilingojea papa hapa mpaka alipokuja.” Kisha kasema, “Sasa, huyu hapa.” Kasema, “Bwana, laiti ningalimsikia mtoto wangu

mchanga akisema, ‘Ni—nimeokoka,’” kasema, “itakuwa sawa.” Naye akaomba, kisha akaacha kuomba, akasema, “Amina.”

Akasema, “Waweza kuomba, Kasisi?”

Nikasema, “Naam, Mama, Dada.” Nikaweka mikono yangu juu ya miguu yake, baridi.

²²⁰ Akasimama na kuyapangusa machozi mashavuni mwake, namna *hiyo*, akambusu shavuni. Haidhuru kama alikuwa ni fedheha, alisema, “Mtoto mchanga wa mama.” Sasa, mnaona, hiyo—hiyo ni... Haidhuru alikuwa nini, bado ni mtoto wake mchanga, mnaona, haidhuru. Mnaona, jambo ndilo hilo. Mnawazia juu ya upendo wa mama, sasa, bali Mungu alisema, “Mama huenda akamsahau mtoto wake mchanga, bali mimi siwezi kukusahau.” Mnaona? “Jina lako limechorwa kwenye vitanga vya mkono Wangu.” Yeye anakupenda, usijali, kama unaliamini Neno Lake, endelea tu.

²²¹ Akapiga magoti, nikaweka mikono yangu juu ya miguu yake. Akaendelea kusema, “Uhhh, uhhh, kuna giza humu ndani.” Kasema, “Uhhh, uhhh, giza humu ndani. Loo, Mama!”

Nikasema, “Waweza kuinge naye?”

Kasema, “La, yeye hajui mahali alipo.” Kasema, “Amekuwa tu akifanya hivyo kwa siku kadhaa.”

²²² Nikasema, “Baba wa Mbinguni, sielewi ni kwa nini ndege hiyo ilishuka, sasa nimechelewa sana, sitaipata. Na hapa Wewe umenifanya nishuke huku, na dada huyu anayesimama hapa nje, maskini nyumba hii duni, nimekuja hapa kuninii tu... Sijui ni kwa nini niko hapa, Bwana. Niliendelea tu kufuata...”

Akasema, “Loo, Mama. Loo, Mama.”

Ndipo nikasema... Nikasikiliza kidogo, akasema, “Naam, Mpenzi?”

Kasema, “Mama, nuru inaingia chumbani.”

²²³ Ndipo yapata mwaka mmoja baadaye nilikuwa nikipitia huko Phoenix, nilikuwa kwa garimoshi. Mnajua jinsi sandwichi zilivyo kwenye garimoshi, ni ghali sana, na kitu kidogo sana, kwa hiyo tukaingia Memphis, nami nikaruka, nikajinunulie kifurushi kizima cha sambusa, mwajua, kinidumishe mpaka nitakapofika Phoenix. Na kwa hiyo... Tungekuwa siku hiyo na usiku huo. Nami ningeweza kuzipata pale kwa yapata senti kumi na tano kila moja, mwajua. Basi nikaenda kununua kifurushi kizima cha hambaga. Nami nikaenda kujinunulia... Nikashuka mbio namna *hiyo*, nikamsikia mtu fulani akipaza sauti, “Aloo, Kasisi Branham!”

Nikaangalia kulia, maskini mbeba mizigo amesimama pale, nikasema, “Aloo, hapo. U hali gani, Ndugu?” Nikazidi kwenda.

Akasema, “Ngoja kidogo!” Kisha kasema, “Hivi hunijui mimi?”

Nami nikasema, “La, siamini nakujua, Ndugu.”

224 Akasema, “Unakumbuka wakati mmoja,” kasema, “ulikuja nyumbani kwangu,” kisha kasema, “mama yangu alikuwa amesimama nje kwenye lango lile, akingojea kule chini, huku kusini?”

Nikasema, “Wewe si yule mvulana!”

225 Kasema, “Naam, ndimi.” Akasema, “Mi—mimi si... nimeponywa.” Kasema, “Da—da—daktari tayari amesema mimi mzima.” Kisha kasema, “Isitoshe, bali nimeokoka sasa.”

226 Ni kitu gani? Sikilizeni, enyi marafiki, Mungu hutenda kazi pande zote mbili za mstari. Mungu yuyo huyo ambaye angeweza kumwambia mwanamke huyo, yule Mshunami, Mungu yeye yule ambaye angeweza kunena na kumwambia yule mwanamke kisimani, “Nenda, kamwite mumeo”! Mwanamke yuyo huyo angeweza kugusa vazi Lake kumgeuza Yeye katikati ya watu hao... Yeye ni Mungu.

227 Hebu niwaonyeshe jambo fulani. Nina... Nimeona watu weusi hapa nyuma, naamini, na ndugu wawili, watatu wanaoketi hapa. Sisemi jambo hili sasa, mnaona, bali nikiangalia, neema yoyote ya Mungu, si kwa watawala na wafalme, bali kwa maskini mwanamke mweusi asiye na elimu, anayeishi katika makazi madogo kule chini, neema ya Mungu ambayo ingeweza kuishikilia ile ndege kule chini... .

228 Basi sikilizeni, baada ya kuondoka kwenye nyumba hiyo nilitoka nje na kuchukua tekisi nirudi, nilichelewa yapata saa mbili na nusu, nami nikasema, “Nipeleke kwenye kituo cha tekisi.” La, kutoka kwenye tekisi, si kituo cha tekisi, bali uwanja wa ndege. Nikasema, “Sina budi kupanda ndege ninapoweza.” Sasa, ilikuwa ni huko nyuma mara baada ya vita na ilikuwa vigumu kupata ndege. Nilipoingia, nikaingia ndani, kasema, “Wito wa mwisho, Louisville, Kentucky.”

229 Ilikuwa ni kitu gani? Mungu, kwa ajili ya imani ya mwanamke huyo ambaye labda hakujua ABC zake, naam, alijua ABC zake, “Daima Mwamini Kristo,” [English: “Always Believe Christ.”—Mfa.], mnaona, kwa ajili ya mwanamke huyo, maskini, mwanamke asiye na elimu, hakujua mlo unaofuata ulikuwa unatoka wapi, bali uaminifu wake kwa Mungu aliyempenda, ungeweza kuishusha ndege hiyo, na kuishikilia ndege hiyo mpaka maombi ya imani yalipoombwa juu ya mvulana wake, na ingeweza kumchukua mtu na kumsogeza ili nisiweze kwenda kwenye ile ndege, Roho wa Mungu akinigeuza.

230 Haidhuru unajaribu kwenda namna gani, anakurudisha nyuma. Ukimwingiza Mungu ndani yako, ndugu, huwezi kuipitia barabara hiyo nyingine, Kitu fulani kinakugeuza. Na kushikilia ndege hiyo pale kwa ajili ya jambo hilo, Huyo ndiye Mungu yeye yule aliye katika jengo hili usiku wa leo. Mnaamini? Vaeni silaha zote za Mungu. Mnamwamini Yeye?

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
 Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
 Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
 Kwani alipenda kwanza . . .

Ni Wakristo wangapi humu ndani, inueni mikono yenu?
 Kisha msembe hivi:

Kamwe sitamwacha,
 Kamwe sitamwacha,
 Kamwe sitamwacha,
 Kwani alinipenda kwanza.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Loo, Jinsi Ninavyompenda Yesu—Mh.*]

“Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

²³¹ Mti wa Bibi-arusi, ulichipuka kwenye Pentekoste. Kuna Mti ambao Daudi aliuona, ulipandwa kando ya Mto wa maji, Mto mmoja, Roho Mtakatifu, maji haya yote yakitiririka ndani Yake, karama, karama za kiroho, zikitiririka ndani Yake. Majani yake hayawezi kunyauka, yatazaa matunda yake. Hiyo ni kweli? Kumbukeni, utazaa matunda yake kwa majira yake. Mti huo mkamilifu, Kristo, alikuja. Na wakati alipokuja, ilikuwaje? Walimkata na kumweka juu ya . . . (Labda nimekosa . . . Hapa nimefanya jambo fulani hapa, Ben, nafikiri, papa hapa, Ndugu. Mimi . . .)

²³² Walimkata, wakamtundika juu ya mti wa Kirumi, bali alifufuka tena. Hiyo ni kweli. Yuko hapa leo. Hiyo ni kweli. Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisimama na kuwaangalia wasikilizaji. Maskini mwanamke mmoja alipitia hapo karibu siku moja, wakati alipokuwa akipitia kwenye umati wa watu. Walisema, ma—madaktari wa siku hizo, wanafalsafa na—na makasisi walisema, “Yeye ni mwanatelepathia. Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli.” Wangali wanaishi, hiyo roho inaishi, bali Roho wa Mungu angali anaishi pia. Mnaona? Anakuja kwa ajili ya Bibi-arusi Wake. “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.”

²³³ Ni watu wangapi hapa ndani walio wagonjwa ambao hawanijuu, na wanajua sijui lolote kuwahusu? Inua mkono wako. Kila mahali, kila mahali tu. Hili likimjia mtu kutoka Jeffersonville, ama mtu fulani ninayemjua, lisahau, achana nalo. Inua mkono wako, useme, “La, ondoka.”

²³⁴ Sijawa na . . . Ninahisi tu Uwepo Wake, ninajua Yeye yupo hapa. Sikilizeni, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu,” Mnaona? Ilikuwa ni kitu gani? Wakati kama huko Sodoma. Angalieni upotovu, kama ilivyokuwa katika Sodoma, dhambi ya Sodoma, angalieni taifa hili, angalieni mataifa mengine.

²³⁵ Nilikuwa nikisoma gazeti hapa wakati fulani uliopita huko Los Angeles, imeongezeka asilimia arobaini mwaka jana, Wasodoma. Kwa nini? Wanawake wamejianika na kadhalika, mpaka chanzo asili cha mwanamume kimebadilishwa, Wasodoma. “Ilikuwa katika siku za Sodoma . . .”

²³⁶ Angalieni, wakati Lutu, mtu mwenye haki, na jamaa yake walipokuwa kule chini, alifanyika meya wa mji, ama aliketi langoni na alikuwa hakimu, msomi mkuu, lakini hizo dhambi zilitesa nafsi yake nyenye haki kila siku.

²³⁷ Siku moja, kabla tu ya wakati wa mwisho, Ibrahimu, lile Kanisa teule, alitwa atoke, halikuvingia Sodoma, lilikuwa nje ya Sodoma. Sasa, angalieni matabaka haya matatu ya watu, daima, daima kuna mwaminio, anayejifanya mwaminio, na asiyeamini miongoni mwa watu; hao ni Ibrahimu, Lutu, na Msodoma. Sasa, angalieni, kila mmoja alikuwa na ujumbe. Kulikuwa na Malaika watatu waliomjia Ibrahimu, Kanisa teule, wawili wao walishuka kwenda Sodoma na kuwatoa Lutu na mkewe na binti zake, mkewe akageuka, Wasodoma wakateketezwa.

²³⁸ Wawili kati yao, Billy Graham wa kisasa na Oral Roberts, jumbe zake zilishuka zikaingia Sodoma, zikihubiri Neno, zikiwapofusha kwa Neno. Kutokuliamini Neno, wewe ni kipofu. Kuhubiriwa kwa Injili humpofusha asiyeamini, na hivyo ndivyo Billy Graham na hao wainjilisti mashuhuri wanavyofanya, kupofusha.

²³⁹ Lakini kulikuwa na Mmoja aliyekaa na Ibrahimu, Mteule, Yeye alimpa ishara. Mnakumbuka, alikuwa Abram siku moja kabla ya hapo, ama mbili, naye Sara alikuwa S-a-r-a-i, lakini sasa ni I-b-r-a-h-i-m-u na S-a-r-a. Mnaona? Kwa hiyo Huyu aliyeketi pale, yule Mnenaji, Yeye alisema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Binti mfalme.

Kasema, “Yuko hemani.” Nalo hema lilikuwa nyuma ya Malaika.

²⁴⁰ Akasema, “Ibrahimu,” sasa kumbukeni, Sara alikuwa na tisini na Ibrahimu mia moja, tisini na tisa, akasema, “Mimi nitakuzuru.” *Mimi*, kiwakilishi nafsi hapo. “Nitakurudia kwa muhula wa uhai, ile ahadi niliyokwambia.” Kwa maneno mengine, “Sara atamzaa mtoto huyu mchanga.”

²⁴¹ Ndipo akacheka hemani, mnaona, alikuwa mzee, akasema, “Mimi, nipate raha na bwana wangu?” Ibrahimu, mumewe. Kisha kasema, “Yeye ni mzee pia.” Mbona, yeye. . . Walikuwa, kama mume na mke, labda hawakuwa mume na mke kwa miaka ishirini. Mnaona? Walikuwa wazee hivyo, ulikuwa umepita. Kasema, “Mimi?” Naye akacheka.

Naye Malaika, huku amegeuza mgongo Wake, akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Vipi kuhusu hilo? Hiyo ni telepathia? “Kwa nini Sara akacheka?”

Sara akatoka mbio na akasema, “Sikucheka.” Ilikuwa ni kwa sababu aliogopa.

Akasema, “Naam, ulicheka.”

²⁴² Yeye angaliangamia papo hapo kama isingalikuwa kwa ajili ya Ibrahimu, mumewe, yeye alikuwa ni sehemu yake. Nalo Kanisa lingeangamia sasa hivi, kama lisingalikuwa ni sehemu ya Kristo, kwa kutokuamini Kwake. Hawezi kufanya hivyo. Asingeweza kumchukua Sara kwa sababu ya Ibrahimu, Yeye hawezi kuliwajibisha Kanisa kwa sababu ya Kristo, ile Damu ingali ipo, mnaona, hiyo ni kweli, sehemu yake.

²⁴³ Sasa, angalieni, Ye- . . . Basi angalia kile alichomwita Mtu huyu. Lutu, uh, Lutu, hao Malaika walimwongoza Lutu nje. Angalia, Ibrahimu alitoka akaenda kuabudu kwa Malaika huyu, naye akamwita, Elohimu. Ilikuwa ni kitu gani? Mtu huyo alikuwa vipande vya nyama ya ndama, mwana-kondoo, ama, nda—ndama, Naye akanywa maziwa na akala mkate, labda ugali, pia, akaoka keki mekoni ambayo Sara alioka. Naye akala mkate, akanywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, kisha akala ndama wa ng’ombe, hiyo ni kweli, huku amesimama pale, Ibrahimu. Naye Ibrahimu alimwita, Elohimu, anapaswa kujua, yeye alikuwa ndiye, aliyezungumza Naye. Angalieni kama hiyo si kweli, Elohimu, herufi kubwa B-w-a-n-a, sawa na hapo mwanzo.

²⁴⁴ Ilikuwa ni kitu gani? Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Elohimu, Neno, hapo mwanzo, atadhihirishwa katika mwili wa kibinadamu kama Yeye alivyodhihirishwa kule. Whiu! Haleluya! Elohimu, si, nilikuwa, MIMI NIKO. Mnaona?

²⁴⁵ Yuko hapa usiku wa leo, vivyo hivyo. Mnaamini hilo? Kweli mnaamini? Kama mtu fulani katika jengo hili nisyemjua, kama ni Roho Mtakatifu, kama mtaninii tu. . . Ni wangapi wanaoamini ya kwamba mwanamke huyo alimgusa Yesu, si kimwili, bali imani yake ilimgusa? Mnaona? Hiyo ilikuwa ni nini? Vazi, hakika. Kipofu Bartimayo, jambo lile lile. Mnaona? Imani yake ilimsimamisha. Ninataka kuhubiri kabla sijaondoka, *Ndipo Yesu Akasimama Kimya*, na sasa, Bwana akipenda.

Vazi hili kubwa, vazi la Kipalestina, alijipenyeza, maskini mwanamke huyu dhaifu na kuligusa vazi Lake. Akasema, “Kama ninaweza kufanya hivyo. . .”

Na wote wakisema, “Rabi,” “Nabii,” “Mdanganyifu,” chochote cha zaidi walichokuwa wakimwita, mwajua, umati uliochanganyika.

Kwa hiyo alikuwa anaenda pale na Yeye akasema, akasimama, kasema, “Ni nani aliyenigusa? Ni nani aliyenigusa?” Kasema, “Mtu fulani alinigusa.”

Kasema, “Loo, kila mtu anakugusa.” Petro akamkemea, kasema, “Jamani, Mtu wa hadhi yako, na kusema, ‘Ni nani aliyenigusa?’”

²⁴⁶ Kasema, “Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu. Nguvu zilinitoka.” Akaangalia kwenye huo umati wa watu akamwona maskini yu—yule mwanamke, ndipo akasema, “Imani yako imekuokoa.”

²⁴⁷ Sasa, Biblia ilisema, katika Kitabu cha Waebrania, ya kwamba Yesu Kristo, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu (Hiyo ni kweli?), anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Angetendaje kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Atende vile vile alivyofanya wakati huo, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule. Biblia ilisema Yeye ni yule yule. Mnaamini hilo? Vema, basi, huwezi kulikwepa Neno, Neno lilisema hivyo.

²⁴⁸ Sasa, hivi sisi. . . ? Una imani ya kutosha kumgusa? Kama ungeweza kumgusa, basi nitajitolea Kwake, na kumwacha Yeye anitumie na kukutumia kuleta imani kwa kusanyiko lote. Hiyo ni changamoto, sivyo? Wewe amini hilo. Unaamini hilo?

²⁴⁹ Je, waweza. . . ? Je, ingeimarisha imani yako kumwona Elohimu, si wewe, si mimi, bali Yeye? Ni kitu gani? Neno. Ni kitu gani? Ulinzi, silaha, silaha za Mungu, Neno la Mungu lililodhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, mwili wako, mwili wangu, kuziona kazi za Mungu. Amina. Ninaamini hilo.

²⁵⁰ Baba wa Mbinguni, labda nilikosea, labda nilitoa changamoto isiyo sahihi. Kama nimefanya hivyo, Bwana, Wewe nisamehe, sikukusudia kufanya hivyo. Lakini inaonekana kana kwamba ni Kitu fulani kinachoniongoza kufanya hivyo. Na kama Huyu ni Wewe, Baba, ambaye nina hakika Ndiye, jitambulishie Mwenyewe sasa, kusudi watu wapate kujua mambo haya ninayonena, nikiwa bado sina elimu, hata hivyo ni kweli. Hayo ni Maneno Yako. Tujalie, Baba. [Unabii unatolewa—Mh.]

²⁵¹ Amina. Mnasikia hilo? Mnakumbuka wakati. . . Jeshi lilikuwa likija wakati mmoja naye Roho wa Mungu akashuka juu ya mtu fulani, na kumwambia jinsi ya—jinsi ya kushuka kwenda kule, akaketi njiani, na jinsi wangelipiga jeshi hilo. Nao wakafanya hivyo. Wakati, ninaamini ilikuwa hivyo, Daudi, sivyo, alipokuwa akizungumza? Mmojawapo? Ndipo Roho akashuka juu ya mmoja wa hao watu na kuwaambia jinsi ya kutoroka. Mlisikia yale huyo aliyosema dakika chache tu zilizopita? “Nitafuteni Mimi.” Yeye ni Neno, dumuni na Neno. Neno linaahidi jambo hili. Sasa, ninajaribu kufanya nini? Kuliadini Neno la Mungu.

²⁵² Sasa, sininii. . . Ninawajua baadhi yenu watu hapa, bali ninyi ombeni. Kama ikishuka juu ya yeyote wenu ninyi watu ninaowajua, tafadhalini, watu wanaotoka Jeffersonville, na

huku karibu ninaowajua, msiombe. Acheni tu iende wakati huu, acheni iwe ni watu nisiowajua. Mnaona, ninyi niombeeni tu, ninawahitaji.

Hebu kidogo, upesi imekuja. Iweni na kicho.

²⁵³ Yupo maskini mama mmoja aliyeketi papa hapa mkono wangu wa kulia, ameweka lesu kinywani mwake. Hatufahamiani, nadhani. Sikujui, Yeye anakujuu. Vema.

Kuna mwanamke anayewasiliana na Mungu ambaye simjui. Yeye hanijui, wala mimi simjui, bali Roho Mtakatifu anatumia sote wawili.

²⁵⁴ Sasa, ulikuwa ukiombea jambo fulani. Ikiwa Roho Mtakatifu atanifunulia kile ulichokuwa ukiombea, kama alivyomfanyia yule mwanamke, “Kutokwa kwako na damu,” mnaona, ungeamini ungekuwa huru?

²⁵⁵ Ni shida ya kiroho inayokusumbua. Hiyo si ni kweli? Kama ndivyo, inua mkono huo. Haitakusumbua tena. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Hilo lingekusaidia? Mildred Rose, mwamini Mungu. “Kama tu ukiamini. . .” Hata hutoki hapa, unatoka Carolina Kusini. Ni kweli. Wewe amini tu, usiwe na shaka. Unaona?

²⁵⁶ Hilo lilimgusa yule mama aliyeketi moja kwa moja nyuma yake. Yeye pia ni mgeni kwangu, lakini Mungu anatumia sote wawili. Uko kwenye shida; kuna kivuli cheusi juu ya huyo mwanamke. Simjui, yeye ni mgeni. Mama anayefuata, ameinua mikono yake *hivi*, lakini, naam, um-hum. Unaamini Mungu anaweza kunifunulia shida yako ni nini? Ungeniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Ungeamini? Wako ni ugonjwa wa wasiwasi. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hautakusumbua tena sasa, imani yako imekuokoa.

²⁵⁷ Unatoka katika nchi hii, unatoka mahali panapoitwa Fayetteville. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi Harrison, basi unaweza kwenda nyumbani, ukaponywe.

Unaamini?

²⁵⁸ Huyu hapa mama ameketi, ameketi papa hapa, akiniangalia. Mimi ni mgeni kwa mwanamke huyu. Wewe ni mgeni kwangu, Dada? Vema. Unaniamini mimi kama nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Unaamini? Kama Mungu atanifunulia shida yako ni nini, utaamini kwa moyo wako wote? Una shida nyingi sana, kwanza una shinikizo kuu la damu, pili una ugonjwa wa moyo, jambo lingine karibu uingine wazimu. Pia unaomba upate kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua lesu yako. Unaamini Mungu anakujuu? Vema, bwana, Bibi Jackson, vema, nenda nyumbani, ukaponywe.

Unaamini?

²⁵⁹ Huyu hapa maskini mama ameketi, ameketi hapa juu akilia. Kwa namna fulani yeye ni mnene, ametengeneza nywele zake namna *hii*, na amevaa nguo nyeupe, ameketi moja kwa moja hapo juu. Mimi ni mgeni. Unaombea jambo fulani. Hiyo ni kweli. Maskini mama huyo hapo, hatufahamiani, sikujui, Mungu anakujua. Unaniamini mimi kuwa mwonaji Wake, ama, mtumishi Wake? Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Unataka kurudi Charlotte, ukaponywe? Huh? Bibi Hines? Nawe unataka mtoto, sivyo? Amini kwa moyo wako wote, unaweza kumpata mtoto wako. Vema.

Unaamini kwa moyo wako wote? Ni wangapi wenu wanaoamini?

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

²⁶⁰ Usininii. . . Unafurahia jambo hilo? Loo, jamani! Ni kitu gani? Roho Mtakatifu. Yuko hapa pamoja nanyi. Hiyo hapo tena. Hebu—hebu na tuamini tu. Shikaneni mikono, shikaneni, wasilianeni, shikaneni mikono. Hili, kusudi mpate kujua ya kwamba Roho Mtakatifu yupo hapa.

²⁶¹ Sasa, sikilizeni, enyi marafiki, hakuna mtu hapa ndani aliye na ufahamu wowote wa kiroho asiyejua sasa kwamba hisia ndogo ya kigeni inapitia kwenu. Ni nini Hiyo? Hiyo ni Neno la Mungu, Hiyo ni Mungu katika umbo la Roho, Neno. Neno, Mungu akiwaimarisha. Mnaona? Msikose kuamini sasa, aminini.

Nimemwona mtu ambaye ndiyo kwanza aponywe kule nyuma ugonjwa wa tezi kibofu. Mungu akubariki, Ndugu. Yote ni. . .

Kisukari, huyo mama, sahau hicho, nenda nyumbani, umepona.

Inaenda tu kila mahali kote jengoni. Mnaamini?

²⁶² Sasa, Biblia ilisema. . . Sikilizeni, Biblia ile ile inayoahidi, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya,” hivi ndivyo alivyofanya, vema, Biblia iyo hiyo inasema hivi, kwamba, “Ikiwa wao. . . Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao,” ninyi nyote ni waaminio, mmewekeana mikono, “wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya.”

²⁶³ Baba wa Mbinguni, tunajua ya kwamba Shetani ameshindwa. Jemadari wetu Mkuu, Yesu Kristo, yupo. Hili hapa Neno Lake likidhihirishwa, limedhihirishwa na Uwepo wa Roho Mtakatifu. Ni Roho Mtakatifu akitenda kazi ndani yetu, Roho Mtakatifu Yeye yule aliyetushushia Moto wa Kipentekoste, akatushushia lugha za Kipentekoste, akatushushia fasiri ya Kipentekoste, ameweka, ameweka kanisani, mitume, manabii, walimu, wainjilisti. Na hapa kwenye mkutano huu mkubwa

unaoendelea, ambapo walimu, wainjilisti, na karama zinatenda kazi kila mahali, tunakuona Wewe, Bwana.

²⁶⁴ Tunajua tuko katika wakati wa mwisho, nao watu wanahitaji nguvu. Shetani anawashambulia, nami ninaweka Neno la Mungu mikononi mwao sasa hivi, mioyoni mwao. Tunamshinda Shetani kwa Neno hili.

Toka ndani ya watu hawa katika Jina la Yesu Kristo!
Angalia mikono yao, angalia imani yao, Mungu.

Shetani, umeshindwa, waache, katika Jina la Yesu. Toka, ninakuapisha kwa Mungu aliye hai.

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza (Unaamini hilo?
Unaamini Yeye anakupenda?)
. . .kununua (Inua mikono yako na uninii
tu . . .) . . .wokovu
Mtini Kalvari.

Nampenda, nampenda, (Loo, Mungu asifiwe!)
Kwani alinipenda kwanza (Alifanya nini?)
. . .kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Ninaweza, nitaamini, kweli nitaamini;
Ninaweza (Ondoka, Shetani.), nitaamini, kweli
nitaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli nitaamini
Kwamba Yesu ananiponya sasa.

²⁶⁵ Ndugu, hivi majuzi, alisema aliota ndoto. Alimwona maskini ibilisi amesimama huko nje, na maskini ibilisi huyo alikuwa akirukaruka, akasema, “Buu!” naye akaruka nyuma. Kila aliporuka nyuma, angekuwa mdogo zaidi na ibilisi angekuwa mkubwa zaidi. Na kila wakati angepiga mayowe “Buu!” yeye angeruka nyuma, naye ibilisi angekuwa mkubwa zaidi.


²⁶⁶ Naye alijua ilimbidi kupigana naye, kwa hiyo akawazia, “Sina budi kutafuta kiti ama kitu fulani,” akaona Biblia. Ndipo ibilisi akasema, “Buu!” naye akasema “Buu!” moja kwa moja, ndipo ibilisi akawa mdogo zaidi. Akasema, “Buu! Buu! Buu! Buu! Buu!” ndipo akamwangusha tu chini.

²⁶⁷ Hicho ndicho kitu cha kumpigia vita, Neno la Mungu. Anapopiga makelele “Buu!” unamjibu “Buu!” Wakati aliposema, “Wewe ni mgonjwa,” sema, “Imeandikwa: Kwa kupigwa Kwake mimi nimepona.” Amina. Utukufu! Ninajisikia kubarikiwa. Hata usiku wa manane bado, bado ninajisikia . . .? . . .Amina.

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao; (Haleluya!)
Mmoja wao, mmoja wao,

Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Njoo, ndugu yangu, utafute baraka hii
Itakayousafisha moyo wako na dhambi,
Itakayofanya kengele za furaha zilie,
Na itaitia nafsi yako moto;
Loo, inawaka sasa moyoni mwangu,
Utukufu kwa Jina Lake,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, mmoja wao. . . 

62-0607 Kuvaa Silaha Zote Za Mungu
Aberdeen High School
Aberdeen, North Carolina Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org